Bismillah ar-Rahman ar-Raheem

SHAHADA[1]

YALIYOMO

Utangulizi wa mfasiri
Utangulizi wa mfasiri wa lugha ya kiingereza
Utangulizi wa mwandishi
Nafasi ya kalima
Ubora wa kalima
Uchambuzi wa kisarufi wa tamko la imani
Nguzo za kalima
Shuruti za kalima
Matakwa ya kalima
Mja anaponufaika na kalima na wapi hanufaiki
Athari za kalima

Mwandishi: Shaykh Saalih ibn Fawzaan al-Fawzaan
Mfasiri wa lugha ya kiingereza: Abu Aaliyah Surkheel ibn Anwar Sharif
Kimechapishwa na kusambazwa na:
Message of Islam, P.O.Box 181,
Hounslow, Middlesex TW 59 YX United Kingdom.
Mfasiri katika lugha ya kiswahili: Ummkhalil

[1] Kimechapishwa na Imaam Muhammad ibn Sa'ud University;
Saudi Arabia – Kitengo cha Utamaduni na Uchapishaji -
Chini ya kichwa cha habari: Maana ya hakuna anaepaswa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah;
1409H / 1989CE.

UTANGULIZI WA MFASIRI

Kwa hakika sifa zote anastahiki Allah. Yeye ndie tunaemtukuza; tunamuomba msaada na tunamuomba msamaha. Tunamuomba Allaah atuepushe na uovu wa nafsi zetu na matendo yetu. Yeyote yule aliyeongozwa na Allah hakuna wa kumpoteza na yeyote yule ambaye hajapata muongozo wa Allah hakuna wakumuongoza. Nashuhudia hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah ambaye hana mshirika; na nashuhudia ya kwamba mtume Muhammad swallallahu alaihi wasalaam ni mja na mtume wa Allah.

Hii ni tafsiri ya kitabu kinachozungumzia SHAHADA kilichoandikwa katika lugha ya kiingereza. InshaAllah, mengi kuhusu kitabu hiki tutapata katika utangulizi wa mfasiri wa lugha ya kiingereza na utangulizi wa mwandishi. Ni mategemio yetu, lugha iliyotumika katika kitabu hiki itaeleweka kwa wepesi na ujumbe uliokusudiwa kwa waislamu na jamii kwa ujumla utafika. Tunamuomba Mola aliyetukuka atujalie tuifahamu shahada hii na yale yote yaliyonasibiana nayo katika ufahamu sahihi na tuwe ni wale wenyekutekeleza shurti zake kama vile Allaah anavyopenda.

Sehemu yeyote ya makala hii inaruhusiwa kutoa nakala (kopi) na kusambaza bure kwa dhumuni la kufikisha elimu kwa waislamu na wasiokuwa waislamu kokote walipo. Hairuhusiwi kubadilisha chochote au kufanya biashara/kuuza sehemu yeyote ya makala hii bila kuwasiliana na mwandishi.

Vile vile, napenda kuwashukuru wale wote waliochangia kwa njia yeyote ile katika kuboresha kazi hii. Shukran za dhati kwa *akhee* Said Baa'del, Abu Maaladh; kwa kujitolea kupitia na kuhariri kazi hii. Tunamuomba Mola mtukufu amjaze kheri zisizokuwa na kifani. Vile vile shukran kwa *abuu* Adam na *Abuu* Othman kwa kutoa mapendekezo ambayo yamechangia kuboresha zaidi kazi hii, *JazakumAllahu kheiran*.

Mwisho, namuomba Allaah mwingi wa kusikia na kuona, aipokee kazi hii na aijalie iwe ni yenye manufaa katika uislamu na waislamu. Na sifa zote anastahiki Allah, Mola wa ulimwengu, na sala na salaam zimshukie kiongozi wetu Muhammad; familia yake, swahaba zake na wale wote wenye kuwafatiliza katika mambo ya kheri mpaka siku ya mwisho.

Umm Khalil
29 Jumaada ath-Thaanee 1429 AH
04 July, 2008

UTANGULIZI WA MFASIRI WA LUGHA YA KIINGEREZA

Kwa hakika sifa zote anastahiki Allah. Yeye ndie tunaemtukuza; tunamuomba msaada na tunamuomba msamaha. Tunamuomba Allaah atuepushe na uovu wa nafsi zetu na matendo yetu. Yeyote yule aliyeongozwa na Allah hakuna wa kumpoteza na yeyote yule ambaye hajapata muongozo wa Allah hakuna wakumuongoza. Nashuhudia hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah ambaye hana mshirika; na nashuhudia ya kwamba mtume Muhammad swallallahu alaihi wasalaam ni mja na mtume wa Allah.

Ama baada ya hayo:

Allaah aliyetukuka amesema:

Jua ya kwamba laa illaha illallaah (hakuna apasae kuabudiwa kwa haki ila Allaah), na omba maghfira kwa dhambi zako na (dhambi) za waislamu wanaume na waislamu wanawake." [Soorah Muhammad 47:19]

Hiki, kwa rehema za Allaah, ni tafsiri ya kitabu cha kiarabu: Laa illaaha illallaah; maana yake, matakwa yake na athari yake kwa binadamu na jamii kwa ujumla, alichoandika, Sheikh wetu mpendwa, Shaykh Saalih al-Fawzaan – Allaah amuhifadhi na amjalie aendelee kunufaisha *ummah*.

Japo hiki kitabu kilishatafsiriwa huko nyuma, imeonekana kuna umuhimu wa kufanya marekebisho na uboreshaji. Pia, Kuliko kupitia tafsiri ya awali, imeonekana ni bora kufasiri upya kabisa, ambayo matokeo yake sasa yapo kwenye mikono ya wasomaji wetu watukufu.

Zaidi ya hayo, kuna vipengele katika makala halisi ya kitabu ambavyo tumeonelea vinahitaji ufafanuzi zaidi ambao utakua unamanufaa au hata ni muhimu zaidi kwa msomaji.Hivyo basi maalezo zaidi yameeambatanishwa katika dondoo. Maalezo haya mengi yake yemechukuliwa katika maandishi na uchapishaji wa vitabu vingine vya sheikh mwenyewe- ikitegemewa maalezo haya yatamsaidia msomaji katika kufahamu na kuridhia umuhimu wa mada hili.

Kwa hakika, elimu kuhusu kalima, laa ilaaha illaalaah ni msingi mkuu katika misingi ya dini ya kiislamu. Hivyo basi, elimu hii ni elimu muhimu na bora kabisa, kwa sababu umuhimu wa kufahamu jambo fulani unatagemea unaambatana na nini (Sharhul-Aqeedatit-Tahaawiyyah (1/5), Imaam lbn Abil-'Izz).

Hadithi (yale yaliyonukuliwa kwamba mtume sallallahu alaihi wasallam amefanya, au ameyashuhudisha) zote zilizotumika marejeo yake yamenukuliwa na zimeonyeshwa pia uhakika wake kwa kunukuu maulamaa wanasema nini na mtiririko wake.

Napenda kuwashukuru wote ambao wamesaidia katika kutafsiri kitabu hiki na uchapishaji wake. Shukran za pekee kwa Dr. 'Abdullaah al-Farsee; amabae uhariri wake

na mapendekezo yake yamechangia kwa kiasi kikubwa kuboresha kitabu hiki. Kwa hakika mtume *sallallahu alaihi wasallam* amesema: “Yule ambae hashukuru binadamu, hamshukuru pia Allaah, (Sahihi, at-Tarmidhi/2021/kutoka kwa Abu Sa’eed *radhiyallahu anhu*. (Sheikh Albani ametaja kuwa ni sahih katika Sahiha/416)

Mwisho, namuomba Allaah kwa majina yake mazuri aipokee hii kazi na aijalie iwe ni yenye manufaa katika uislamu na waislamu. Na sifa zote anastahiki Allah, Mola wa ulimwengu, na sala na salaam zimshukie kiongozi wetu Muhammad; familia yake, swahaba zake na wale wote wenye kuwafatiliza katika mambo ya kheri mpaka siku ya mwisho.

ABU ‘AALIYAH SURKHEEL IBN ANWAR SHARIF
21 Rabee’uth-Thaanee 1419H
(15/08/1998CE)
London, England

UTANGULIZI WA MWANDISHI

Kwa hakika sifa zote anastahiki Allah. Yeye ndie tunaemtukuza; tunamuomba msaada na tunamuomba msamaha. Tunamuomba Allaah atuepushe na uovu wa nafsi zetu na matendo yetu. Yeyote yule aliyeongozwa na Allah hakuna wa kumpoteza na yeyote yule ambaye hajapata muongozo wa Allah hakuna wakumuongoza. Nashuhudia hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah ambaye hana mshirika; na nashuhudia ya kwamba mtume Muhammad swallallahu alaihi wasalaam ni mja na mtume wa Allah.

Ama baada ya hayo:

Allah, aliyekamilika, ametuamrisha tumtukuze. Allaah anawasifu wale wenye kumtukuza na anawaahidi malipo makubwa. Allaah ametuamrisha kumkumbuka kila wakati na nyakati zingine maalumu, baada ya kumaliza baadhi ya ibada alizotushurutisha. Allah aliyetukuka amesema:

"**Mwishapo kusali kuweni mnamkumbuka Allaah (vilevile) msimamapo na mkaapo na (mlalapo) ubavu**." [Soorah an-Nisaa 4:103]

Na Allaah, amesema:
"**Na mwishapo kutimiza ibada zenu (za hija),basi mtajeni Allaah kama mlivyokuwa mkiwataja wazee wenu; bali mtajeni zaidi (Allaah)**." [Soorah al-Baqarah 2:200]

Allaah ameamrisha kukumbukwa wakati wa kuzuru nyumba ya Allaah (Hajj: Maka). Kuhusu hili, Allah aliye juu kabisa amesema:

"**Na mtakaporudi kutoka Arafat mtajeni Allaah penye Mash'aril-Haram. Na mkumbukeni kama alivyokuongozeni. Na hakika zamani mlikuwa miongoni mwa waliopotea.**" [Soorah al-Baqarah 2:198]

Allaah aliyetukuka amesema pia:
"**Na kithirisheni kulitaja jina la Allaah katika siku zinazojulikana (fadhila zake)juu ya yale aliyowaruzuku, nao ni wanyama wenye miguu minne**." [Soorah al-Hajj 22:28]

Na tena Allaah aliyetukuka amesema:
"**Na mtajeni Allaah katika zile siku zinazo hesabiwa**" [Soorah al-Baqarah 2:203]

Allaah ameamrisha sala ili apate kutajwa kama alivyosema:
"**Kwa hakika Mimi ndiye Allaah, hakuna aabudiwaye kwa haki ila Mimi,Basi niabudu na usimamishe sala kwa kunitaja**." [Soorah Taa Haa 20:14]

Mtume sallallaahu 'ala yhi wa sallam amesema:

> "Siku za kuchinja (at-tashreeq) ni siku za kula, kunya and kumkumbuka Allaah." (Muslim/1141) kutoka kwa Nubayshah al-Hudhalee *radhiyallahu anhu*. Imaam

an-Nawawee amesema katika Sharh Saheeh Muslim [8/15]: “Siku za at-tashreeq ni siku tatu kuanzia siku ya Idd al hajj)

Allaah aliyetukuka, amesema:

“**Enyi mlioamini! Mkumbukeni Allaah kwa wingi. Na mtukuzeni asubuhi na jioni**.” [Soorah al-Ahzaab 33:41-42]

Mtajo (dhikr) bora kabisa ni: Hakuna anaepaswa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah, peke yake bila mshirika; kama ilivyosimuliwa kutoka kwa mtume *sallallahu alaihi wasallam* ambaye amesema:

> “Dua bora ni dua inayoombwa siku ya ‘Arafah; na dua bora ambayo mimi na mitume wengine tunaiomba ni: Hapana anaipaswa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah, peke yake bila mshirika na ufalme, utukufu na sifa zote anastahiki yeye peke yake.” (at-Tirmidhee (3585). Zaynud-Deen al-’Iraaqee, katika Takhreejul-Ihyaa (1/254-255) amesema ni hadith hasan).

Hivyo basi, kwa sababu hii kalima ya laa ilaaha illallaah ndio bora kabisa kulinganisha na dhikr nyingine na kwa sababu si kalima ambayo inatamkwa tu bali inabeba: -hukumu, shurti, maana na matakwa- Nimeamua kuchagua kalima hii kuwa ndio makusudio ya mjadala wangu. Natumaini Allah aliyetukuka, atatufanya sote tue ni wale ambao wanashikamana na kalima hii kithabiti; wanaofahamu maana yake kikamilifu, na wanaotenda matendo yaliyo wazi na yaliyofichika kama yanavyoambatana na matakwa ya kalima hii.

Mjadala huu utachambua kalima katika vipengele vifuatavyo:

- Daraja lake katika maisha ya muislamu
- Ubora wa kalima
- Uchambuzi wa maana ya kalima
- Nguzo zake
- Shurti zake
- Maana yake na matakwa yake
- Wakati gani inamnufaisha yule anayeitamka na wakati gani haimnufaishi
- Athari zake

Hivyo, nasema, huku nikimuomba Allaah aliyetukuka anisaidie:

DARAJA YA KUKIRI NA KUTAMKA SHAHADA

Ni kalima ambayo waislamu wanaitamka katika maisha yao ya kila siku; kama vile, kuwafahamisha waislamu wakati wa sala (adhana), kuwaita katika kisamamo cha sala (‘iqaamah), hutuba zao na maada zao. Ni kalima ambayo kwa sababu yake, mbingu na ardhi zikatandazwa, na viumbe wakaumbwa na ndio sababu Allaah akatuma mitume, vitabu vyake na sheria zake. Vile vile kwa sababu yake (kalima) mizani na vitabu vya kunukuu amali za binadamu vikawekwa na pepo na moto vikabainishwa.

Kutokana na kalima, viumbe wanagawanyika katika kundi la waaminifu na makafiri, waja wema, na waja waovu. Ni mzizi wa kuwepo viumbe, hukumu, malipo na adhabu. Ni kwa sababu ya haki yake ndio viumbe wakaumba na wataulizwa haki yake na watalipwa kutegemeana na utekelezaji wake. Kwa sababu yake, uelekeo wa kibla wakati wa kuswali ukawekwa, na ni juu yake ndio msingi wa dini ulipo, na kwa sababu yake dini ya Allaah inapiganiwa (jihadi).

Ni haki ya Allaah juu ya waja wake, na ndio ufunguo wa peponi. Kuhusu hii kalima, umma uliotangulia na uliofuata wataulizwa. Kwa hakika hakuna mja atakae simama mbele ya Allaah bila ya kuulizwa maswali mawili, nayo ni: Nini ulikuwa unaabudu na vipi ulipokea ujembe wa mitume? Jibu la swali la kwanza linapatikana kwa kufahamu laa ilaaha illallaah; kuwa na ilmu nayo, kushikamana nayo, na kufanya matendo ambayo yanaambatana nayo. Na jibu la swali la pili ni kukubali na kushuhudia Muhammad sallallahu alaihi wasallam ni mtume wa Mwenyezi Mungu, Allaah; Yaani kuwa na ilmu juu yake, kushikamana nayo na kuwa mtiifu juu ya yake [Shaykh Saalih al-Fawzaan (hafidhahullaah) amesema katika Sharhul- Aqeedatil Waasitiyyah (uk.8): “Kushuhudia Muhammad ni mtume wa Mwenyezi Mungu, Allaah, kunahitaji kuwa na imani juu yake, kuwa mtiifu juu yake kwa yale aliyoamrisha, kukaa mbali na yale aliyoyakataza, kuamini lolote lile alilolisema na kumfuata katika yale yaliyoamrishwa kama sheriah ya Allaah, (Zaadul-Ma’aad (1/34) ya Imaam Ibn al-Qayyim)].

Hii kalima ni mpaka kati ya kufuru na Uislamu. Ni tamko la taqwa/uchamngu (kalimatut-taqwaa), mshiko thabiti wenye kuaminika (al-’urwatul-wuthqaa) na ni tamko ambalo Ibraaheem alaihis-salaam amelifanya kama:

“Na akalifanya neno hili ni neno lenye kubaki katika kizazi chake ili warejee kwa Allaah huku wakiwa wamefanya toba na watiifu” [Soorah az-Zukhruf 43:28]

Ni kalima ambayo Allaah Mwenyewe ameshuhudia, kama vile malaika na wenye ilmu walivyoshuhudia. Allaah aliyekuwa juu kabisa amesema:

“**Mwenyeezi Mungu ameshuhudia ya kwamba hakuna apase kuabudiwaye kwa haki ila yeye tu. Na malaika na wenye ilmu (wote wameshuhudia hayo);(Yeye) ndiye Mwenye kusimamisha uadilifu. Hakuna apase kuabudiwaye kwa haki isipokuwa Yeye, Mwenye nguvu na Mwenye hikma.” [Soorah Aal-’Imraan 3:18]**

Ni tamko la kujitakasa na kujenga ikhlasi (kalimatul-ikhlaas), ushahidi na mwito katika haki, shuhudio la kujinasua katika shirki[2] na ndio sababu ya viumbe kuumbwa. Allaah aliyetukuka amesema:

“Sikuwaumba majini na watu ili wapate kuniabudu.” [Soorah adh-Dhaariyaat 51:56]

Kwa sababu yake, mitume wametumwa, vitabu na nyaraka za Allaah vikateremshwa, kama vile Allah alivyosema:

“Na hatukumtuma kabla yako Mtume yoyote ila tulimfunulia ya kwamba hakuna apasae kuabudiwaye ila mimi,basi Niabuduni.” [Soorah al-Anbiyaa 21:25]

Allaah aliyetukuka amesema pia:

“Huwateremsha Malaika na Wahyi wenye kubeba hukumu zake/sheria kwa juu ya anaowataka katika waja wake kwamba "Waonyeni (viumbe)kuwa hakuna apasae kuabudiwa isipokuwa Mimi basi Niogopeni (Kwa kuacha yale yote Allaah aliyoyakataza na kutokuwa watiifu).” [Soorah an-Nahl 16:2]

---

[2] (Shaykh, hafidhahullah, amesema katika Kitaabut-Tawheed (uk.9): “Shirk ni kumshirikisha Allaah aliyetukuka na kingine chochote katika ufalme wake (ruboobiyyah), Uungu Wake na kuabadiwa kwake (uloohiyyah). Shirki inajitokeza zaidi katika imani ya Yeye peke Yake ndie anaepasa kuabudiwa na katika kutekeleza ibada; kama vile kuomba mizimu, mashetani, makaburi n.k au kufanya vitendo vya ibada si kwa ajili ya Allaah, kwa mfano kuchinja, kula kiapo, kupenda, kuogopa, kuwa na khofu, kuwa na matumaini kwa kingine chochote na si kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Allah.- Na shirk ndio dhambi kubwa katika madhambi yote.”

Imaam as-Sa’dee, rahimahulaah, ameandika maana ya shirki kwa kirefu na undani katika al-Qawlus-Sadeed (uk.48):

“Maana ya shirk kubwa na maelezo yake ambayo yanabeba vipengele vyote na vidokezo ni: Mja wa Allaah, anaelekeza aina yeyote ya ibada au sehemu ya ibada kwa kingine chechote zaidi ya Mwenyezi Mungu, Allaah. Hivyo, imani, tamko au tendo lelote ambalo kisheria linahesabika ni ibada, likielekezwa kwa Allah peke yake basi huko ndio kumkwepesha Allaah (tawheed), kuwa na imani juu yake, na kutenda matendo kwa ajili yake peke yake (ikhlaas); Lakini, vikiwa vinaelekewa/vinafanywa kwa ajili ya kingine chechote zaidi ya Allaah basi hiyo ni shirk kufr. Hivyo basi kuwa katika huu mstari wa kukukingana na shirki kubwa, mpaka ambao hautoi nafasi kwa lolote lile.

Hivyo hivyo, maana ya shirki ndogo ni: nia yeyote ile ama tamko au tendo lolote lile ambalo halijafikia daraja la ibada, lakini linafungua mlango utakaosababisha shirki kubwa

Ibn ‘Uyaynah, (radhiyallahu anhu) amesema: “Allaah hakufadhili juu ya viumbe vyake zaidi ya takrima ya kuifahamu laa ilaaha ilallaah. Kwa hakika, laa ilaaha illallaah ni kwa waja wa peponi, kama vile maji ya baridi kwa viumbe duniani [Imusimuliwa na Ibn Rajab katika Kalimatul-Ikhlaas (uk.53)]

Yeyote yule atakayeitamka hii kalima, mali yake, damu yake ni vyenye kustahiki kulindwa, kinyume na yule ambaye anaikana, kwa sababu si mali wala damu yake vinavyostahiki kulindwa. Imesimuliwa katika mojawapo ya vitabu sahihi vya hadithi, kwamba mtume sallallahu alaihi wasallam amesema: “Yeyote yule atakayesema: laa ilaaha illallaah na kukana kuabudiwa kwa kingine chochote zaidi ya Allah, basi mali yake na damu yake ni tukufu na hesabu yake ni juu ya Allaah, (Muslim, 37).”

Ni jambo la mwanzo linalomlazimu kafiri kutamka akitaka kuwa muislamu[3], kwa sababu mtume sallallahu alaihi wasallam alipomtuma Mu’aadh Yemen, alimwambia:

[3] Imaam Ibn al-Mundhir, (rahimahullaah) amesema katika al-Awsat (uk.73-75): “Kwa wale waliobeba ilmu sahihi wanakubaliana kwamba pale kafiri atakapofikia umri wa kubaleghe na mwenye akili timamu kisha akakiri laa ilaaha illallaah; na kwamba Muhammad ni mja na mtume na kila alichokuja nacho Muhammad sallallahu alaihi wasallam ni haki/kweli na kisha akijinasua nafsi yake katika dini yeyote inayokwenda kinyume na dini ya kiislamu- basi yeye ni Muislamu

Ama Kuamini kwamba wajibu wa kwanza wa binadamu ni kumfahamu Allaah kwa kutumia dalili za kiakili na kudhamiri mambo - ambayo wengi wa wahubiri wa kiislamu wa siku hizi wanaitilia mkazo – hili ni kosa kubwa!

Imaam Ibn Abil-’Izz, rahimahullaah, amezungumzia hili suala katika Sharhul Aqeeda at - Tahaawiyyah (1/23): “Jambo ambalo ni sahihi katika wajibu wa mwanzo wa mja ambaye amekomaa akili (mukallaf) ni kukiri laa ilaaha illallaah. Wala sio kudhamiri kiakili, au kutaka kudhamiri mambo, au kuwa na shaka – ambayo ndivyo wanavyo amini viongozi wengi wenye kustahiki kulaumiwa na wenye kuingiza matamshi ambayo ni bidaa (al-kalaamulmadhmoom). Wakati, maulamaa kutoka katika waja wema waliotangulia (Salaf) wote walikubaliana kwamba wajibu wa mwamzo wa binadamu kuamrishwa ni kukiri kalima ya imani (shahaadatain).”

Imaam an-Nawawee, rahimahullaah, amesema vile vile kama yaliyotangulia hapo juu katika Sharh Saheeh Muslim (1/187): “Katika hili ni ushahidi wa maulamaa wanoaminika na wengi wa waja wema waliotangulia (Salaf) na maulamaa waliofuatia (khalaf), kwamba pale mja atakapokubali Uislam ndio dini ya haki ya kufuata- Akiwa na imani thabiti isiyokuwa na shaka ndani yake- Basi hili ni tosha kwa yeye kuwa muumini. Na atukuwa ni muumini kati ya waja wanaomkwepesha Mwenyezi Mungu, Allah (Tawheed). Na wala si wajibu kwake kumfahamu Allaah kwa kutumia dalili za watu wa falsafa (almutakallimoon) au kumfahamu Mwenyezi Mungu, Allaah aliyetukuka kutoka kwao.

Hili ni kinyume na wale wanaoweka sharti la mja kuwa muislamu/ waja wenye kuelekeza nyuso zao kibla, ni lazima maudhui ya wana falsafa yatumike. Ufahamu huu, ambao unatumika na kikundi kimojawapo cha waislamu kinachofahamika kama Mu'tazilah na waislamu wenzetu wanaochukua elimu kutokana na ufahamu hafifu wa binadaam (Ahlal kalaam), ni wazi kabisa unakwenda kinyume, kwa sababu jambo linalohitajika ni uhakika na ukweli ambao umeshapatikana, na kwa sababu mtume sallallahu alaihi wasallam ameonyesha uaminifu kwa aliyotumwa kufikisha na amalikamilisha hilo, kwani hakutufahamisha kufahamu kwa akili ni shurti.

Shaykhul-Islaam Ibn Taymiyyah nae amesema katika Dar'ut-Ta'aarudil-Aql wan-Naql (8/21): "Kuna kikundi kinachoaamini kwamba kumtambua Allaah kwa kutumia ufahamu wa akili ni wajibu, na haitawezekana kufika kiwango hicho isipokuwa kwa kupitia njia hii, hivyo basi wamefanya ni wajibu kwa kila mtu kutumia akili kumtambua Allah. Na ufahamu huu umesambazwa katika ummah huu wa kiislamu na Mu'tazilah pamoja na wale wanaowafuata nyao zao."

Ibn Hajr al-'Asqalaanee, rahimahullaah, pia amepinga ufahamu huu potovu katika Fathul-Baaree (13/437) akisema: "Maneno yake yanakubaliana kama alivyosimulia Aboo Daawood kutoka kwa Ibn 'Abbaas: "Manamume mmoja alimuuza mtume wa Mwenyezi Mungu, Allah, sallallahu alaihi wasallam: Je ni Allaah amekutuma kwamba tushuhudie hapana anaepaswa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah na kwamba tuache kuabudu al-Laat and al-'Uzzaa (majina ya sanamu zilizokuwa zinaabudiwa)? Mtume wa Allaah akajibu: "Ndio." Basi mwanamume huyu akaukubali uislamu."

Msingi wa hadithi hii unapatikana katika masimulizi ya Bukhari na Muslim kuhusu riwaya ya Dammaam ibn Tha'labah. Katika hadithi ya 'Amr ibn 'Abasa, kama ilivyosimuliwa na Muslim, 'Amr amesema: "Nilikwenda kwa mtume sallallahu alaihi wasallam nikasema: Wewe ni nani? Akajibu: Mtume wa Mwenyezi Mungu, Allaah. Nikasema: Je ni Mwenyezi Mungu, Allaah amekutuma? Akajibu: Naam. Nikasema: amekutuma nini? Akajibu: Kumkwepesha Mwenyezi Mungu, Allaah katika ibada na kutomshirikisha na chochote kile katika kumwabudu Yeye. ['Amr akaingia uislamu]." ... Pia kuna barua ambazo mtume sallallahu alaihi wasallam alizituma kwa Hercules, Chosroes na wafalme wengine, kuwaita katika kumkwepesha Allaah katika ibada (tawheed)

Riwaya hizi na nyingine zenye kubeba maana moja (mutawaatir) zinathibitisha kwamba, mtume sallallahu alaihi wasallam alipokuwa akiwaita makafiri katika kumwamwini Mwenyezi Mungu, Allaah na kuhakikisha kwa kile alichokuja nacho; hakuongeza juu yao kufanya uchambuzi wa dalili za kiakili. Hivyo basi, yeyote yule aliyepokea wito wake, alikubalika kama muislamu bila ya kuhakikasha kama amechambua au amefahamu kwa kutumia ufahamu wa kifalsafa."

Jambo muhimu la kuzingatia: Shaykh Muhammad Ibn Maani' amesema katika Sharhul

> “Unakwenda kwa watu waliopewa kitabu (Wakristo/Mayahudi), hivyo basi waite kwanza katika kumwabudi Allaah peke yake (Bukhari/1458; Muslim/31& 29).”

Hivyo basi, katokana na yaliyotangulia utaona sehemu ya kalima, laa ilaaha illallaah katika dini, umuhimu wake katika maisha ya muislamu na ndio jambo la mwanzo ambalo ni wajibu kwa binadamu kulifahamu kwa sababu ndio msingi wa amali na ibada zote.

‘Aqeedatis- Safaareeniyyah (uk.61): “Baadhi ya maulamaa wamesema: Kuzingatia mambo kiakili (nadhr) ni wajibu katika baadhi ya mazingira na si yote, na ni wajibu kwa baadhi ya watu lakini si wote.

UBORA WA KALIMA

Kalima (Laa illaha illaallaha) inabeba sifa nyingi zenye kuonyesha ubora wake na mbele ya Allaah ina nafasi kubwa kabisa. Yeyote yule atakayeitamka kwa haki/ukweli, ataingia katika bustani ya peponi na yeyote yule ambae ameitamka tu, bila ya ukweli katika nafsi yake, mali yake na damu yake vitalindwa hapa duniani lakini atabainishwa siku ya malipo na Allah Subhanallahu wa ta'ala. Ni kalima fupi yenye maneno machache, mepesi kutamka lakini ni yenye kubeba uzito mkubwa katika mizani.

Imesimuliwa kutoka kwa Ibn Hibbaan, vile vile na al-Haakim ambaye ameipitisha kama hadithi sahihi, kutoka kwa Abu Sa'eed al-Khudree *radhiyallahu anhu*, kwamba mtume wa Allaah *sallallahu alaihi wasallam* amesema:

> "Nabii Musa amesema: Ewe Mola wangu! Nifundishe mimi jambo ambalo litanifanya nikukumbuke na nikuombelee juu yake. Allah akasema: Ewe Musa! Sema laa ilaaha ilallaah. Nabii Musa akasema: Ewe Mola wangu! Waja wako wote wanatamka neno hili. Allaah akasema: Ewe Musa! Ikiwa mbingu zote saba na vyote vilivyobeba kasoro Mimi, ardhi zote saba vikawekwa upande mmoja wa mizani na upande mwingine ikawekwa kalima ya laa ilaaha ilallaah, basi laa ilaaha illallaah itakuwa nzito zaidi ya vyote hivyo. (Imesimuliwa na Ibn Hibban katika Sahih yake (# 2324) na al-Haakim katika al-Mustadrak (1/528))

Japo uhakika wa hadithi hii umepingwa na baadhi ya maulamaa wa hadithi- kama alivyo elezea Shaykh Shu'ayb al-Arna'oot katika ufafanuzi wa Sharhus-Sunnah (5/55) ya al-Baghawee – ukweli wa ubora wake umetajwa katika hadithi iliyosimuliwa na Ahmad (2/169), kutoka kwa 'Abdullaah ibn 'Amr *radhiyallahu anhu*. Hii hadithi imepitishwa usahihi wake na mmojawapo wa maulamaa mashuhuri katika elimu ya hadithi (muhaddith) katika karne hii Shaykh Muhammad Naasirud-Deen al-Albaanee, katika kitabu as-Saheehah (no.134).

Hadithi hii inathibitisha kwamba kalima ya laa ilaaha illallaah ndio bora kuliko aina zote za dhikr kama vile ilivyosimuliwa pia na 'Abdullaah ibn Umar:

> "Dua iliyo bora ni ile itakayo letwa katika siku ya Arafa, na bora ya dua ambayo mimi au mitume waliotumwa kabla yangu walisema ni : Hakuna apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah ambaye hana mshirika na ni kwake Yeye ufalme wote na Ndiye anayestahiki sifa zote na ni Mwenye uwezo juu ya kila jambo." (at-Tirmidhee (no.3585). Zaynud-Deen al-'Iraaqee, katika Takhreejul-Ihyaa (1/254-255) amesema ni hadith hasan).

Zaidi ya hayo, uzito wa kalima katika mizani unaonyeshwa pia katika hadithi iliyosimulia na at- Tirmidhee, ambayo amesema ni sahihi,- vile vile na an-Nasaa'ee, na al-Haakim ambao wapeipitisha usahihi wa hadithi kwa kutumia masharti ya Muslim – Kutoka kwa 'Abdullaah ibn 'Amr, kutoka kwa mtume *sallallahu alaihi wasallam*, ambae amesema:

‘Mmoja wapo wa wafuasi wangu ataitwa mbele ya watu wote siku ya malipo; nyaraka tisini na tisa zenye nukuu ya matendo yake zitafunguliwa; kila nyaraka inaurefu zaidi ya upeo wa macho. Kisha ataulizwa: Je unakana kwa lolote lile (madhambi yaliyonukuliwa)? Basi mtu huyu atajibu: Hapana Ewe Mola wangu. Kisha ataulizwa je unasababu yeyote ya kujitetea au unajambo lolote zuri ulilotenda? Mtu huyu katika hali ya kutetemeka kwa uwoga atajibu: Hapana. Kisha ataambiwa bali unayo mambo mema na hakuna dhulma itakayofanyika siku ya leo. Basi kipande cha nyaraka nyingine kitatolewa ambacho kitakuwa kimebeba ushuhudio wa kalima laa ilaaha illallaah na ushuhudio wa kwamba Muhammad ni mja na mtume wa Allaah. Basi mja huyu atasema: Ewe Mola wangu, utafananisha vipi kipande hiki cha nyaraka na nyaraka zote hizo? Ataambiwa: Hautafanyiwa dhulma. Basi nyaraka zitawekwa upande mmoja wa mizani na upande mwingine itawekwa kile kipande cha nyaraka kilichobeba kalima, upande wa nyaraka tisini na tisa utakuwa mwepesi na upande wa kipande cha nyaraka kilichobeba kalima utakuwa mzito.”[Sahihi: Imesimuliwa na at-Tirmidhee (no.2641), kutoka kwa ‘Abdullaah ibn ‘Amr *radhiyallahu anhu*; naye Shaykh al-Albaanee ameipitisha kama hadithi sahihi katika as-Saheehah (no.135)].

Kwa hakika ubora wa kalima hii ambayo haifanani na kalima yeyote inabebeba sifa nyingi. Haafidh Ibn Rajab ametaja baadhi ya sifa za kalima katika makala aliyoipa jina la Kalimatul-Ikhlaas. Ambazo ni:-

- Ni thamani ya kulipa ili kupata bustani ya peponi (jannah)
- Yeyote yule ambaye tamko lake la mwisho kabla ya kufa ni laa ilaaha illallaah ataingia peponi.
- Ni uokuvu wa kutoingia motoni
- Sababu ya kusamehewa madhambi
- Ndio amali bora kuliko amali zote njema
- Inafuta madhambi yote
- Ina uhusha imani iliyopandikizwa katika nafsi
- Ina beba uzito zaidi kulinganisha na dhambi yeyote katika mizani
- Inavunja mipaka yote inayomzuia mja kukutana na Allaah aliyetukuka
- Allaah anampa sifa ya ukweli yeyote yule atakayeitamka kalima
- Ndio kalima bora ambayo mitume wote wameitamka
- Ndio dhikr bora kuliko dhikr zozote, ndio amali bora kuliko zote na ndio amali ambayo thawabu zake zinazidishwa zaidi kuliko amali zingine.
- Tamko la kalima ni sawa na kumwachia huru mtumwa
- Ni kinga ya kumzuia Shaytaan
- Ni njia yakupata salama na giza la kaburini na zahma la siku ya kukusanywa viumbe vyote (al-hashr)
- Itawatafautisha waumini na waje wengine siku watakaofufuliwa kutoka makaburini
- Milango yote minane (8) ya peponi itafunguliwa kwa yule mja aliyeshuhudia kalima na itakuwa ni chaguo lake kuingia mlango autakao. Hata kama mja atalazimika kuingia motoni kwanza kutokamana na upungufu katika utekelezaji wa amali njema; kwa hakika iko siku atotolewa motoni na ataingia peponi.

Hizi ndizo sifa kuu ambazo Ibn Rajab amezitaja katika makala yake kuhusu ubora wa kalima, na katika kila sifa ametoa dalili zake. (Tazama, kalimaatul-ikhlaas, uk. 54-66)

UCHAMBUZI WA KISARUFI WA TAMKO LA IMANI

Kwa kuwa kuelewa maana ya maelezo (matamshi) inategemea kujua/kufahamu uchambuzi wa kisarufi, wanazuoni –Allaah awape rehma juu yao – wameweka uangalifu mkubwa wa uchambuzi wa kisarufi wa laa illaaha illallaah. Hivyo wamesema:

Neno **laa** [ambalo linamaanisha: Hapana] linajulika kama sehemu pekee ya kukana/kukanusha. Neno **ilaah** ni nomino/jina inayoshabihiana, ambayo imenyambulishwa na inayokuwa na kuhusishwa kwa vipasho na maneno yaliyoondolewa (taqdeer). Katika swala hili taqdeer linamaanisha "haqq" (haki) likimaanisha hakuna mwenye haki au anayestahili kuwa **illaah**. Fungu la maneno **illallaah** (isipokuwa Allaah), ni pekee kwa kanusho la awali (hakuna anayestahili kuabudiwa) na katika swala teule (isipokuwa Allaah).

Maana ya **illaah** ni kile kioneshi kiambatanasho na ibada. Ni kile ambacho moyo unakipenda, heshimu sana na kuabudu; Katika hicho kutarajia kupata faida au kwa ajili ya kinga dhidi ya madhara. (Hivyo maana ya kalima ni hakuna kinachostahiki kuabudiwa isipokuwa Allaah)

Ni kosa kufikiri kwamba umboyai (taqdeer) ni neno: kuwepo (mawjood) au anayeabudiwa [ma'bood] kwa sababu [tamko la imani] basi itamaanisha: hakuna uungu uliopo isipokuwa Allaah, au hakuna kinachoabudiwa isipokuwa Allah]; Hali ya kuwa kuna vitu vingi viilivyopo vinavyoabudiwa mbali na Allah, kama vile sanamu, makaburi na vitu vingine. Walakini Mmoja pekee mwenye haki ya kuabudiwa ni Allaah na yeyote mwingine anayeabudiwa kando yake ni batili.

Na hivi ndivyo nguzo (arkaan) mbili za laa ilaaha illallaah zinavyofahamisha:

NGUZO ZA KALIMA

Kalima imebeba nguzo mbili: Nguzo ya kwanza ni nguzo ya kukana (nafee), na nguzo ya pili ni nguzo ya kukubali kwa yakini na thabiti (ithbaat). Nguzo ya kukana inamaanisha kakana hakuna sifa ya Uungu na ibada (ilaahiyyah) yeyote inayostahiki kuelekezwa isipokuwa kwa Allaah, Aliyetukuka. Na nguzo ya kukubali kwa uyakini na uthabiti, inamaanisha kuwa na yakini sifa ya Uungu na aina zote za ibada zinastahiki kuelekezwa kwa Allaah, aliyetukuka; kwani ni Yeye peke yake ambaye ndiye Mungu wa kweli. Hivyo basi kila wanacho amini makafiri kuwa na sifa ya uungu yenye kuabudiwa ni uongo na batili:

“Hayo ni kwa sababu Mwenyeezi Mungu ndiye mwenye kustahiki kuabudiwa; na wale wanaowaabudu badala yake (Mwenyeezi Mungu) hao ni batili.” [Soorah al-Hajj 22:62]

Imaam Ibn al-Qayyim amesema: “Ubora wa laa ilaaha illalaaah katika kukubali kwa yakini sifa ya uungu na matendo ya ibada kuwa anastahiki Allaah peke yake ni bora kabisa zaidi ya kukiri tu Allah ni mmoja wa illah. Hii ni kwa sababu kusema Illah inamaaninsha Allaah, inakuwa haijakanusha kuabudiwa kwa kingine chochote. Na hii ni tafauti na kusema Hapana apasae kuabudiwa kwa haki ila Allaah, kwa sababu, sentensi hii ya pili inaonyesha ni wajibu kuonyesha mpaka wa sifa ya Uungu na matendo yote ya ibada ni kwake Yeye, Allaah, peke yake.

Vile vile, wale wenye kufasiri al-Ilaah- inamaanisha: Yule ambaye anauwezo wa kuumba na kuanzisha jambo bila ya kuwa na vifaa au mahitajio (al-qaadir ‘alaalikhtiraa’) kwa hakika wamefanya makosa makubwa. Shaykh Sulaymaan ibn ‘Abdullaah amesema katika uchambuzi wa Kitaabut-Tawheed: “Kama itachukuliwa kwamba maana ya (ilaah) na (ilaahiyyah) kama ilivyoelezwa katika ufahamu sahihi, itajibiwa vipi hoja ya wale wenye kusema maana ya al-Ilaah ni: Yule mwenye uwezo wa kuumba na kuanzisha uhai pasipokuwa na chochote? Jibu ya hoja hii inagawanyika katika sehemu mbili kama ifuatavyo:

Kwanza: Maana hii ni bida’a, kwani hakuna ulamaa yeyote wala wataalamu katika lugha ambao wamebeba maana hii; bali ufahamu wa maulamaa na wataalamu wa lugha unakubaliana na maana sahihi kama ilivyoelezwa hapo nyuma. Hivyo basi, mtazamo huu ni batili.

Pili: Hata kama maana hii itakubalika, basi ni sehemu tu inayoelezea sifa za mwenye kustahiki Uungu. Kwani kwa hakika mwenye kustahiki Uungu ni lazima awe na uwezo wa kuumba na kuanzisha uhai pasina kuwa na chochote. Na kama hatakuwa na sifa hii basi huyo si mungu wa kweli mwenye kustahiki sifa ya Uungu hata kama atakuwa anahesabika kama Mungu kwa baadhi ya watu.

Vile vile ni lazima na muhimu ifahamike kwamba haina maana yeyote yule ambaye anaamini kwamba Mungu ni yule ambaye anauwezo wa kuumba na kuanzisha uhai, basi

atakuwa ameingia katika uislamu[4]. Ufahamu huu haujawahi kusemwa wala kufahamika kutoka kwa maulamaa. Na kama ikiaminika hivi, basi waarabu ambao hawakuamini wangehesabika kama waislamu[5].

---

[4] Shaykh amesema katika Bayaan Haqeeqatut-Tawheed (uk.19): "Baadhi ya watu wanaelezea maana ya ilaah ni: Ni Yule mwenye uwezo wa kuanzisha maisha na kuumba pasipo kutumia nyenzo zozote. Hivyo maana ya laa ilaaha illallaah katika ufahamu wao ni: Hakuna Mwenye uwezo wa kuanzisha na kuumba isipokuwa Allaah; Na huu ni upotuvu mkubwa! Yeyote yule atakae elezea maana ya kalima katika ufahamu huu tu, hajakubali na kuwa na yakini tofauti kama vile ambavyo makafiri walivyoamini. Kwani makufari walikuwa na yakini hakuna mwenye uwezo wa kuumba, kuruzuku na kudumisha, kujalia uhai, kuzuia/kusababisha mauti isipokuwa Allaah- kama vile Allaah, aliyetukuka, alivyowazungumia kuhusu wao (makafiri) katika qur'an. Na Allah hakuwataja kama wao ni waislamu (kwa sababu wanabeba imani hii).

Ni kweli maana hii inaingia katika maana ya kalima laa ilaaha illallaah kwa ujumla lakini haibebi maana halisi ya kalima." (Pia unaweza kurejea tafsiri ya Soorah al-Qasas; aya ya 70 katika Tafseer ya Imaam at-Tabaree (20/102) au Tafseer ya Ibn Katheer (3/408)).

[5] Shaykh, hafidhahullaah, ameelezea zaidi hili suala katika Mujmal 'Aqeedatus-Salafis-Saalih (pp.10-12), ambapo amesema: "Imani ya kwamba ufalme na miliki ya vyote vilivyomo duniani na mbinguni ni juu ya Mwenyezi Mungu Allaah (tawheed ar-ruboobiyyah) inakubaliani na fitrah ya binadamu, ni vigumu kwa binadamu yeyote kukana hili; kwani hata ibilisi-ambaye ndio kiongozi wa ukafiri- amesema:

"Akasema:"Mola wangu! Kwa sababu umenihukumu kupotea, basi nitawapambia (viumbe vyako upotofu)(upotevu)katika ardhi na nitawapoteza wote" [Soorah al-Hijr 15:39]

Na amesema pia:

"**Na-apa kwa haki ya utukufu wako,…" [Soorah Saad 38:82]**

Kutokana na aya hizo, inaonyesha ibilisi amekiri pia ufalme na miliki ya vyote (ruboobiyyah) ni juu yake Allaah peke yake. Zaidi ya hayo ibilisi amekula kiapo pia juu ya ufalme wa Allah. Hivyo hivyo, makafiri wote pia (mfano Aboo Jahl, Aboo Lahab na viongozi wengine wa makafiri ambao walimpinga mtume swallallahu alaihi wasalaam. Na walikuwa si wenye kuamini na ambao hawajaongozwa.

Allaah aliyetukuka amewazungumzia makafiri kama hawa kwa kusema:

"Na ukiwauliza ni nani aliyewaumba? Kwa yakini watasema, "Ni Allah" Basi ni wapi wanakogeuziwa?" [Soorah az-Zukhruf 43:87]

Na tena Allah aliyetukuka amesema:

“Sema: "Ni nani Mola wa mbingu saba na Mola wa Arshi kuu?" Watasema:"Ni Allah."Basi sema je hamumuogopi?" [Soorah al-Mu’minoon 23:86]

Allaah aliyetukuka amesema pia:

“Sema: "Ni nani mkononi Mwake umo ufalme wa kila kitu, Naye ndiye alindaye, na hakilindwi (chochote) kinyume Naye, kama mnajua (jambo nambieni hili)." Watasema:"(Uwezo huo) ni wa Allah" Sema:"Basi vipi mnadanganywa (na shetani) mkadanganyika” **[Soorah al-Mu’minoon 23:89-90]**

Tena Allaah aliyetukuka amesema:

“**Sema: "Ni nani anayekuruzukuni kutoka mbinguni (kwa kuleta mvua) na katika ardhi (kwa kuotesha mimea)? Au ni nani anayemiliki masikio (yenu) na macho (yenu)? Na nani amtoaye mzima katika mfu na kumtoa mfu katika mzima? Na nani atengezaye mambo yote?" Watasema ni Allah. Basi sema: "Je hamuogopi? (Mnawaabudu wengine pamoja naye)!" [Soorah Yoonus 10:31]**

Hivyo basi, utakuta ya kwamba wameafikiana na yote haya, juu ya ukweli kwamba wakipatikana na misukosuko yeyote au wakati wa shida walikuwa wakimuomba Yeye Allah peke yake. Na hii ni kwa sababu walikuwa wanajua hakuona uokovu katika balaa lolote isipokuwa Allah aliyetukuka ndie atake waongoa; Na pia walikuwa wanafahamu miungo yao na masanamu hawana uwezo wa kuwaokoa katika dhuruba yeyote.

Allaah aliyetukuka amesema kuwahusu wao:

“Na inapokufikieni taabu katika bahari, hupotea wale mnaowaita (waungu, hamuwataji) isipokuwa Yeye tu (Mungu wa haki). Lakini anapokufikisheni salama nchi kavu, mnakengeuka. Ama mwanaadamu ni mwingi wa kukanusha (neema za Allah).” [Soorah al-Israa 17:67]

Hivyo, yeyote yule ambaye atakuwa na yakini kwamba imani juu ya Allah ni kuamini tu kwamba “Hakuna Mwenye uwezo wa kuanzisha na kuumba isipokuwa Allaah (tawheed ruboobiyyah)”; basi atakuwa hajaingia katika Uislamu wala hata okolewa katika moto. Kwani – tukichukulia mfano wa makafiri wa Quraish- Walikuwa na yakini juu ya ufalme wa Allah (tawheed ruboobiyyah) lakini uyakini wao haukuwafanya wawe waislamu, na Allah amewakinisha kama wao ni waja wenye kuamini sanamu (mushrikina) na ni makafiri (kuffaar) na hukumu juu yao ni kuingia motoni milele japo wamebaba uyakini wa tawheed ruboobiyyah!

Kutokana na yaliyotangulia tunaona makosa ya wale – kwasababu ya kuchukua ufahamu wa akili tu (ahlul-kalaam) katika vitabu vyao kuhusu imani katika uislamu- wanaelezea tawheed kama vile ni kuamini TU kwamba Allaah yupo na ndiye aliyeumba, mwendeshaji n.k. Hivyo basi tunasema kwa wenye kubeba upotovu huu wa imani juu ya Allah kwamba; Hii siyo imani ambayo mitume wametumwa kuifundisha na Allaah, kwa

Na kama maulamaa waliofuatia wanabeba ufahumu huu, basi ifahamike wanafanya makosa, kwani ufahamu huu unapingwa na mafundisho ya qu'an na sunna vile vile na kwa kutumia akili (Rejea, Tayseerul- 'Azeezil-Hameed (uk.56-57).

---

sababu washirikina (mushriks) na makafiri (kufar) – na kwa hakika hata Ibilisi – walikuwa tayari wana imani juu ya haya [ufahamu wa tawheed ar-ruboobiyyah]." Imaam Ibn Abil-'Izz, rahimahullaah, amesema katika Sharhul-'Aqeedatit- Taahawiyyah (1/28-29): "Tawheed ambayo mitume wamewaita watu na ambayo ndio sababu ya vitabu kuteremshwa ni tawheed ya kumkwepesha Allah katika ibada (tawheedul-ilaahiyyah) bila ya kumshirikisha na chochote; na hii tawheed inabeba tawheed ar-ruboobiyyah. Kwa hakika waarabu waliokuwa wanamshimrikisha Allah wakati wa mtume waliamini tawheed ar-ruboobiyyah na muumba wa mbingu na ardhi ni Mmoja tu." Mwisho, Imaam at-Tabaree ameeleza katika Jaami'ul-Bayaan 'an Ta'weelil Qur'aan (13/50-51) kwamba Ibn 'Abbaas radiallaahu anhu, amesema: "Ukiwauliza nani aliyeumba mbingu na ardhi, watasema ni: Allaah. Lakini japo na kuamini huku, wanaabudi vingine pasipokuwa Yeye (Allaah)".

SHURUTI ZA KALIMA YA IMANI

Haitamnufaisha yule ambaye anaitamka tu pasipo kutimiza masharti saba yafuatayo[6]:

Shuruti la kwanza: Ufahamu (al-'ilm) wa maana yake, nini inakanusha na nini inakubaliana nayo. Kama mja ataitamka kalima bila ya kufahamu maana yake wala kufahamu nini jukumu lake basi haitomnufaisha na chochote kwa sababu atakuwa hajaamini mahitajio ya kalima. Na atakuwa hana tofauti na yule ambaye anazungumza lugha ambayo haielewi maana yake.

Shuruti la pili: Yakini (al-yaqeen), ambayo inamaanisha kuwa na uhakika wa hali ya juu, juu ya kalima bila wasiwasi au dhana yeyote.

Shuruti la tato: Ikhlasi (al-ikhlaas), kumkwepesha Allah katika ibada bila ya kumshirikisha na chochote. Na huu ndio mwelekeo wa laa ilaaha illallaah

Shuruti la nne: Ukweli (as-sidq), jambo ambalo linapinga unafiki (nifaaq). Kwa hakika wanafiki wanaitamka hii kalima kwa ndimi zao lakini ndani ya nafsi zao hawajaamini matakwa ya kalima.

Shuruti la tano: Kuwa na mapenzi (al-mahabbah) juu ya kalimah hii na kuwa na mapenzi pia kwa yale yote ambayo yanalazimika kutekelezwa. Na hii inapinga unafiki katika utekeleji wa matakwa ya kalima.

Shuruti la sita: Utekelezaji katika hali ya unyenyekevu (al-inqiyaad), kwa kutimiza haki zake- kutimiza yale yote ambayo ni wajibu kwa muislamu kuyafanya- kwa ajili ya Allah subhanAllahu wa ta'ala huku ukitegemea kumfurahisha Yeye tu; kwani hii ndio mahitajio ya kalima.

Shuruti la saba: Kuikubali (al-qabool) kalima, na wala si kuikana. Na shuruti hii inatimizwa kwa kufanya yale matendo ambayo Allah Subhanahu wa ta'ala ameyaamrisha na kuacho yote aliyoyakataza.

Maulamaa wamechambua hizi shuruti kutoka katika marejeo ya Qur'an na Sunnah ambayo yanafafanua zaidi ni jinsi gani kalima hii muhimu kabisa inatakiwa ifahamike, na jinsi haki zake na mipaka yake inavyotakiwa kulindwa na vile vile ifahamike siyo kalima inayo tamkwa tu bila maana yeyote.

[6] Baadhi ya maulamaa kama mfano Shaykh 'Abdul-'Azeez bin Baaz katika Majmoo' Fataawaa wa Maqaalaat Mutanawwi'ah (7/56) na Shaykh 'Abdullaah ibn Jibreen katika ash-Shahaadataan (uk.77), wameongeza shuruti la nane nalo ni: Kukana kuelekeza ibada yeyote ile pasipokuwa kwa Allaah.

MATAKWA YA KALIMA YA IMANI

Ni wazi kwa yale yaliyotangulia, kwamba maana ya laa ilaaha illallaah ni: Hapana apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Yule mmoja tu mwenye sifa ya Uungu, naye ni Allah, subhanAllah wa ta'ala bila ya mshirika na yeyote. Ni Yeye peke yake anayestahiki kuabudiwa.

Hivyo basi, kalima hii yenye uzito mkubwa inamaanisha chochote kile kinachoabudiwa pasinapokuwa Allah, sio mungu wa kweli mwenye kupaswa kuabudiwa, bali yote hayo yanoyochukuliwa kama mungu ni batili. Ni kwa ajili hii maamrisho mengi yenye kuamrisha ibada ielekezwe kwa Allah subhanahu wa ta'ala yanakwenda sambamba na maarisho ya kutomshirikisha na chochote katika ibada. Na ibada yeyote itakayoshirikishwa na chochote pamoja na Allah subhanAllahu wa ta'ala, ibada hiyo inakuwa siyo sahihi:

Allah aliyekuwa juu amesema:

Muabuduni Allaah wala msimshirikishe na chochote." [Sura An-Nisa, 4: 36]

Allah, aliyekuwa juu, amesema tena:
"Basi na yeyote yule anayekana at taaghoot na akamuamini Allaah bila ya shaka amekamata kishikio madhubuti, kisicho vunjika. Na Allaah ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua." [Soorah al-Baqarah 2:256] (Imaam Ibn-Qayyim rahimahullah, amesema katika I'laamul-Muwaqqi'een (1/53): "At-Taaghoot ni yeyote yule/chochote kile ambacho mja mweingine anazidisha mipaka katika kumwabudu, kumtii na kumfuata (hali ya kuwa yanamfurahisha)."

Allaah aliyetukuka, katika aya nyingine amesema:
"Na kwa hakika kwa kila umma tuliutumia Mtume kwamba: Muabuduni Allaah, na muepuke kuabudu kingene chochote (at Taghoot) pasipokuwa Allaah." [Soorah an-Nahl 16:36]

Mtume *sallallahu alaihi wasallam amesema*:
"Yeyote yule atakayesema laa ilaaha illallaah na akakana kingine chochote kinachoabudiwa isipokuwa Allaah, damu yake, mali yake inakuwa tukufu na mahesabu yake ni juu ya Allaah." (Muslim, #37)

Kila mtume amesema kwa watu wake:
"Enyi kaumu yangu! Muabuduni Allaah. Nyinyi hamna mwingene mwenye kupasa kuabudiwa kwa haki zaid yake Yeye." [Soorah aI-A'raaf 7:59]

Na kuna dalili zingine zaidi ya hizi. Imaam Ibn Rajab, rahimahullaah, amesema: "Kuelezea maana hii na kuifafanua zaidi: Pale mja atakapotamka laa ilaaha illallaah, kutokana nayeye inamaanisha, kwamba hapana apasae kutukuzwa na kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah. Na al-Ilaah ni Yule ambae ni mwenye kuabudiwa na wala si mwenye kukwaswa kwa sababu ya kumuhofia huku ukionyesha mapenzi juu Yake na pia

kwa sababu ya mapenzi, matumaini na mategemeo juu Yake; vile vile kuwa Yeye ndiye mwenye kuombwa katika kutimiza matakwa na kujibu dua. Na haya yote yakielekezwa kwingineko hayatokuwa ni sawa, isipokuwa yakielekezwa tu kwa Allah aliye na Nguvu na Utukufu." (Kalimatul-Ikhlaas (uk. 25))

Hii ndio sababu mtume *sallallahu alaihi wasallam* aliposema kwa makafiri wa ki-Quraysh: **Sema, laa ilaaha illallaah**, walijibu kwa hamaki:

"Amewafanya miungu wote kuwa ni Mungu Mmoja tu anayepaswa kuabudiwa (Allaah)? Hakika hili ni jambo la ajabu!" [Soorah Saad 38:5]

Makafiri hawa walielewa kwamba hii kalima inapinga kuabudiwa kwa chochote na miiungu yeyote na inaweka mpaka wa kumuabudu Allaah peke yake, na walikuwa hawalitaki hili jambo.

Hivyo ni wazi kwamba laa ilaaha illallaah, ikiambatana na mahitajio yake, inamaanisha: Kwamba Allaah peke yake anatakiwa akwepweshe katika ibada na kuabudu vingine pasipokuwa Allah ni lazima viachwe. Kwa mantiki hii, mja atakaposema laa ilaaha illallaah, ana thibitisha kwamba ni wajibu kumkwepesha Allah peke yake katika ibada na wakati huo huo anathibitisha ubatili wa kuabudu kingine zaidi Yake YeYe kama vile masanamu, (waja waliokufa) makaburi, na waja bora na wema.

Ubatili wa wale wanaoabudu wafu makaburini na vinginevyo, unaonyesha ya kwamba, wanaamini kwamba laa ilaaha illallaah inamaanisha tu kuyakinisha kwamba Allah yupo, au Yeye ndiye muumbaji na Mwenye uwezo wa kuanzisha uhai pasina na chochote au maana nyinginezo zenye kubeba maana sawa; ama inamaanisha hukumu na ufalme (haakimiyyah) ni wa Mwenyezi Mungu, Allaah peke yake. Wanafikiri pia yeyote yule mwenyekuamini hivi na mwenye kufafanua laa ilaaha illallaah katika mantiki hii, basi watakuwa wamefikia ukweli wa tawheed – hata kama watakuwa wanaabudu na vingine pamoja na Allah ama wakiamini wakielekeza ibada zao kwa wafu; wakijikurubisha kwao kwa kutambika, kula viapo juu yao, wakifanya tawaafu katika makaburi yao na wakitaka kupata neema (tabarruk) katika ardhi iliyowazunguka!

Watu hawa hawanaufahamu kwamba hata makafiri wa kiarabu walikuwa wamebeba imani hii, na walikuwa pia wanakubali kwa uyakini kwamba Allaah ndio muumba mwenye uwezo wa kuanzisha uhai pasina kuwa na chochote. Walikuwa wakidai kwamba wanaabudu vingine pamoja na Allah wakiamini miiungo yao itawakurubisha kwa Allah subhanAllah wa ta'ala. Hawakuamini kwamba masanamu hayo waliyokuwa wanayaabudu ndiyo yaliyoumba au ndiyo yenye kuruzuku.

Hivyo basi, imani kuwa hukumu yote ni juu ya Allah (haakimiyyah) ni sehemu tu ya maana ya laa ilaaha illallaah, siyo maana halisi na kamili ya laa ilaaha illallaah. Kwa mantiki hii, haitoshelezi kuhukumu kwa sheria za Allah (sharee'ah) katika haki za binadamu, mipaka na adhabu zake (hudood) na mtafarakano, huku shirk katika kumuabudu Allah ambaye ndiye ameziweka hizo sheria zikipuuziwa!!

Na kama maana ya laa ilaaha illallaah ni kama wanavyodai, basi kusingekuwa na mtafaruku baina ya mtume *sallallahu alaihi wasallam* na mushrikun, ambao walikuwa wanaabudu masanamu pamoja na Allaah. Kwa hakika kama mtume *sallallahu alaihi wasallam* angewaambia wakubali kwamba Allaah ndiye Yeye peke yake mwenye uwezo wa kuanzisha uhai ama kukubali kwamba Allah yupo au kama angewafahamisha kwamba wakihukumu kwenye masuala kama vile ya dhuluma katika uhai wa binadamum mali au haki za binadamu watumie sheria za Allah lakini wasitilie maanani suala la kumkwepesha Allaah katika ibada; basi wangekubali kwa haraka ujumbe wa mtume *sallallahu alaihi wasallam*. Lakini hawakukubali, kwa sababu walikuwa wanajua lugha ya kiarabu; hivyo basi walifahamu fika kama wangesema laa ilaaha illallaah, wangekuwa wanakubali ubatili wa kuabudu masanamu na walijua hii kalima sio tu usemi usiokuwa na maana. Na ndiyo sababu baadhi ya kikundi kati yao walisema:

“Amewafanya miungu wote kuwa ni Mungu Mmoja tu anayepaswa kuabudiwa (Allaah)? Hakika hili ni jambo la ajabu!” [Soorah Saad 38:5]

“Na tena Allaah amesema kuhusu wao: “Wao walipo kuwa wakiambiwa waseme laa ilaaha illallaah, wakijivuna. Na wakisema: Hivyo sisi tuiache miungu yetu kwa ajili ya huyu mtunga mashairi mwendawazimu?” [Soorat as-Saafaat 37:35-36]

Na pia walifahamu fika kama wangesema laa ilaaha illallaah, ingekuwa ni wajibu kwao kumkwepesha Allaah peke Yake katika ibada, na kama wangeitamka kalima na huku wanaendelea kuabudu masanamu basi wangekuwa wanapingana baina yao; hivyo walikataa wasije wakahitalifiana.

Lakini, waislamu wa leo wanaobudu makaburi hawapingani na hii maana iliyojificha. Wanasema laa ilaaha iilallaah lakini bado wanapingana na matakwa yake kwa sababu wanabudu wafu na wanajikurubisha katika makaburi na wanafanya ndio sehemu za kufanyia baadhi ya ibada. Hivyo, Ole wao kwa wale waliokuwa na ufahamu finyu juu ya maana ya laa ilaaha illallaah kuliko Aboo Jahl and Aboo Lahab!

Kwa kifupi: Yeyote Yule mwenye kuitamka kalimah hii, huku akifahamu maana yake, akitekeleza mahitajio yake dhahiri na ndani ya nafsi yake, akikana shirki na akiyakinisha kumkwepesha Allah katika ibada zote, bila ya kuwa na shaka katika imani hii kwa kile inachokimaanisha, huku akitekekeza matakwa yake (akifanya yale yote ambayo ni wajibu kwa muislamu- Basi yeye atakuwa ndio mwislamu wa kweli.

Lakini kwa yule ambaye anaitamka kalima hii lakini haamini nini mahitaji yake basi yeye ni munafiki (munaafiq) japo kidhahiri anatekelaza mahitaji ya kalima. Vilevile, yeyote yule anayoitamka kalima kwa ulimi wake lakini matendo yake hayaendi sambamba na maana na matakwa ya kalima basi ni mshirikina mwenye sifa ya kuhitalifisha nafsi yake[7]

[7] Shaykh, hafidhahullaah, ameelezea zaidi katika al-Muntaqaa min Fataawaa (1/9-10)
“Yeyote yule atakayetamka kalima ya laa ilaaha illallaah muhammadur-rasoolallah, atahesabika muislamu na damu yake inakuwa ni tukufu. Kama atafanya yele ambayo yanahitajika kwa mwenye kuikuabali kalima kwa yakini katika nafsi yake na kwa dhahiri

Hivyo basi ni muhimu sana ifahamike, haitoshelezi kuitamka tu kalima bali ni lazima pia kufahamu maana yake, kwani kwa kufahamu maana yake mja atajua ni nini wajibu wake katika kutekeleza matakwa ya kalima. Allaah, aliyetukuka amesema:

“Isipo kuwa wale wanao shuhudia kwa haki, na wana ilmu.” [Soorah az-Zukhruf 43:86]

Na kutekeleza mahitaji ya kalima inamaanisha kumwabudu Allah peke yake bila ya kumshirikisha na chochote, kwani hili ndilo jambo kuu katika matakwa ya kalima. Vile vile katika mahitaji ya laa ilaaha illallaah ni kukubali sheria za Allah (sharee’ah) katika ibada, biashara na lipi ni halali na lipi haramu huku mja akikana sheria nyingine zozote zaidi ya sheria za Allah. Allah aliyekuwa juu kabisa amesema:

“Au hao wanao wanaoshirikiana na Allaah walio watungia dini asiyo itolea idhini Allaah?” [Soorah ash- Shooraa 42:21]

Hivyo basi ni wajibu kuzikubali sheria za Allaah katika ibada, biashara, kuhukumu baina ya binadamu katika mambo ambayo wamekhitilafiana na wakati huo huo kukana sheria zilizotungwa na binadamu. Hii inamaanisha kukana bida’a na yale yote yanayokwenda kinyume na Allaah katika ibada, ambayo yameanzishwa na kusambazwa na waovu kati ya watu na majini. Kwa hakika, yeyote yule atakayekubali kati ya haya (bida’a na mambo yanayokwenda kinyume na matakwa ya Allaah) basi atakuwa anafanya shirki katika utiifu juu ya Allaah, kama alivyosema Allaah katika aya hii:

“Au hao wanao wanaoshirikiana na Allaah walio watungia dini asiyo itolea idhini Allaah?” [Soorah ash- Shooraa 42:21]

---

basi yeye ni muislamu kamili na anabashiriwa habari njema hapa duniani na kesho akhera; lakini akiwa anatekeleza matakwa ya kalima kwa nje tu basi atahukumiwa kama muislamu kutokana na matendo yake japo ndani ya nafsi yake amebeba sifa ya unafiki ambazo Allah ndiye mjuzi zaidi juu yake yeye. Na kama ikiwa mja hatekelezi matakwa ya kalima: laa ilaaha illallaah, na akawa anajitosheleza kwa kuitamka tuu, ama akawa anafanya matendo ambayo ni kinyume na matakwa ya kalima basi hukumu ya kumkufurisha itapitishwa juu yake na atakuwa anahesabika kama kafiri. Na kama atakuwa anafanya baadhi ya matakwa ya kalima na baadhi hayatekelezi basi ni wajibu itazamwe: kama katika matakwa ya kalima anayoyaacha yanapelekesha kwenye kufuru; kama vile kuacha sala kwa makusudi ama kuelekeza ibada kwa kingine chochote isipokuwa Allah, basi atahukumiwa kama kafiri. Lakini ikiwa katika matakwa ya kalima aliyoyaacha hayampelekeshe kwenye kukufuru basi atahukumiwa kama muumini ambaye imani yake ni dhaifu kulingana na lile jambo aliloliacha; kwa mfano, wale wenye kufanya madhambi ambayo hayahesabiki makubwa udhaifu wao katika imani si sawa na wenye kutenda madhambi makubwa (shirki).”

Na Allaah aliyekuwa juu amesema:

“Na mkiwafuata basi hapana shaka nyinyi mtakuwa washirikina.” [Soorah al-An’aam 6:121]

“Wamewafanya makuhani wao na wamonaki wao kuwa ni marabi badala ya Allaah.” [Soorah at-Tawbaa 9:31]

Katika hadithi sahihi mtume *sallallahu alaihi wasallam* mara alipomsomea aya hiyo hapo juu ‘Adee ibn Haatim at-Taa’ee *radhiyallahu anhu*, akasema: Ewe mtume wa Allaah, hatuwaabudu wao makuhani na makasisi. Mtume sallallahu alaihi wasalllam akajibu: **“Je hawajafanya halali kwa yale ambayo Allaah ameyaharamisha, na kisha nanyi mkakubali ni halali? Na je hawakufanya haramu yale ambayo Allaah ameyafanya halali, na kisha nanyi mkakubali ni haramu?** ‘Adee bin Haatim akasemad: Na’am, kwa hakika. Basi mtume *sallallahu alaihi wasallam* akamwambia: “kwa kufanya hivi ni kuwaabudu.” (Hasan: imesimuliwa kwa meneno haya na al-Bayhaqee katika as-Sunanul-Kubraa (10/116) na lbn Taymiyyah ameipitisha kama hadithi hasan katika Majmoo Fataawaa (7/67). Pia imesimuliwa na at Tirmidhee (#. 3094) kwa maneno tofauti kidogo.)[8,9]

---

[8] Shaykh ‘Abdur-Rahrnaan ibn Hasan, rahimahullaah, amesema: “Hadithi hii ni dalili ya kuonyesha kwamba kuwatii makuhani na makasisi katika mambo ambayo yanasababisha kutomtii Allaah ni kumshirikisha Allaah; na hii ni mojawapo ya shirki ambayo Allaah haisamehei (Fathul-Majeed (2/653))

[9] Shaykhul-Islaam Ibn Taymiyyah, rahimahullaah, ameelezea hili suala kwa undani zaidi katika Majmoo’ Fatawaa (7/70-71), amesema: “Wale ambao wanawachukulia makasisi wao kama Mola wao wakiwaatii katika yale wanayofanya halali wakati Allaah ameyaharamisha na katika yale ambayo wanayafanya haramu wakati Allaah ameyahalalisha wamegawanyika katika makundi mawili:

La kwanza: Wanajua [yaani makuhani na makasisi wao] wamebadilisha dini ya Allaah, lakini bado wanawafuata katika hili jambo la kubadilisha (tabdeel). Na kwa kufanya hivyo ina maana wameamini ni halali yale Allaah aliyoharamisha na ni haramu yale Allaah aliyohalalisha kwa kuwafuata viongozi wao huku wakijua wanakwenda kinyume na dini ya mitume wa Allaah. Huku ni kukufuru, ambako Allah na mtume wake wameyakinisha ni shirki- hata kama watakuwa hawasali juu yao au kuwasujudia.

La Pili – Imani yao imejengeka ki sawa sawa katika yapi ni halali na yapi na haramu; lakini wanawafuata katika kumkosea Allaah, basi wanakuwa sawa na waislamu ambao wanafanya matendo ambayo yanamkosea Allaah huku wakifahamu fika wanamkosea Allaah. Watu hawa wanabeba hukumu sawa kama waislamu wanaotenda madhambi. Lakini, kufanya haramu mambo ambayo Allaah ameyahalalisha na kufanya halali yale yaliyo haramishwa ikiwa limefanywa na ulamaa ambaye nia yake ni kumfuata mtume *sallallahu alaihi wasalaam*, lakini haki ya ufahamu sahihi hajafahamu, na anamhofia Allaah kiasi cha uwezo wake, basi Allaah hatamhukumu kama mkosaji. Bali Allaah atamzawadia kwa juhudi (ijthad) aliyofanya ili apate kumtii Mola wake. Lakini mwingine

Vile vile, katika kutekeleza matakwa ya kalima ni wajibu kurejea katika kitabu cha Allah pale hukumu inapotakikana na kukana kurejea katika sheria zilizotungwa na binadamu, kwa sababu ni wajibu kuacha kile chochote kinachokwenda kinyume kutoka katika sheria alizotunga binadamu kwa kuona inamnufaisha zaidi katika mfumo wake wa maisha.

Allaah, aliyekuwa juu amesema:

"Na mkizozana katika jambo basi lirudisheni kwa Allaah na Mtume, ikiwa mnamuamini Allaah na Siku ya Mwisho." [Soorah an-Nisaa 4:59]

Allaah aliyetukaka amesema pia:

"Na mkikhitalifiana katika jambo lolote, basi hukumu yake iko kwa Allaah. Huyo ndiye Allaah ndiye Mola wangu" [Soorah ash-Shooraa 42:10]

Allaah, aliyekamilika, amethibitisha yeyote yule ambaye hahukumu kwa kutumia kile ambacho Allaah amekiteremsha basi atakuwa amekufuru (kufr), amedhulumu (dhulm) and ametenda dhambi (fisq) na imani itakuwa imemtoka. Hivyo basi kama mja akihukumu pasipo kutumia kile ambacho Allaah amekiteremsha (qur'an), huku akiamini sheria ya kiislamu inaruhusu ama akiaamini ni bora zaidi kutumia sheria alizotunga binadamu kuliko sheria za kiislamu (Sheria'h) basi hii ni mojawapo ya shirki kubwa ambayo inakana tawheed na ambayo inabatilisha kalima laa ilaaha illallaah. Lakini, kama anahukumu kwa kutumia sheria alizotunga binadamu huku akiaaamini hairuhusiwi, bali inatakikana kuhukumu kwa kutumia sheria za Allaah, lakini hafanyi hivyo kwa sababu ya kufuata matamanio ya nafsi yake, basi atakuwa anafanya shirk ndogo na kukufuru ambako hakumtoi katika uislamu, lakini inafanya dhaifu mshikizo wake katika kalima ya laa ilaaha illallaah na udhaifu katika kutekeleza matakwa yake (kalima).

Hivyo basi, laa ilaaha illallaah ni mfumo wa maisha uliokamilika. Ni wajibu kwa kila muislamu kutekeleza matakwa ya kalima katika ibada zao na maisha yao vile vile na katika tabia zao. Kalima, sio tu usemi unaosemwa ili kupata neema/rehma au ni usemi tu unaosemwa katika dhikiri za asubuhi na jioni bila ya kufahamu maana yake au bila ya kutekeleza matakwa yake au kwenda kinyume ni kile kilichosisitizwa- kama vile wengi wa waislamu wanayoitamka tu kwa ndimi zao lakini wanakwenda kinyume kama imani zao na tabia zao zinavyoonyesha, hawa kweli hufikiri!

Zaidi ya hayo, katika mojawapo pia ya matakwa ya laa ilaaha illallaah ni kukubali majina (asmaa) na sifa (sifaat) za Allaah; ambayo Yeye mwenyewe amejitambulisha nayo, ama

---

yeyote atakayemfuata hali ya kuwa anafahamu amekosea, lakini bado anamfuata, huku akienda kinyume na mafundisho ya mtume, basi mtu huyu atakuwa naye amefanya shirk katika jambo hilo ambalo Allaah ameliamrisha; haswa ikiwa huyu mtu anafuata matamanio ya nafsi yake huku akililingania kwa ndimi na mikono yake huku akifahamu kwa kutekeleza hilo jambo anampinga mtume *sallallahu alaihi wasalaam*. Hii ni shrki, ambaye anayeifanya anastahiki kuadhibiwa." Hivyo hii ni shirki kubwa ambayo inakwenda kinyume na msisitizo wa kalima tawheed laa ilaaha illallah .

yale ambayo mtume *sallallahu alaihi wasallam* amemwita nayo ama amemwelezea nayo. Allaah aliyetukuka amesem:

“Na Allaah ana majina mazuri kabisa, basi muombeni kwa hayo. Na waacheni wale wanao kataa na kuharibu utakatifu (ilhaad) wa majina yake.” [Soorah al-A’raaf7:180]

Imeelezwa katika Fathul-Majeed:“mzizi wa maana ya neno la ilhaad katika lugha ya kiarabu unamaanisha: Kwenda kinyume na lengo, kuacha maana halisi,…….Majina yote ya Allaah, aliyetukuka, ni majina na sifa zinazomnasibu katika kumwabudu Yeye na vile vile zinaelezea ukamilifu wake. Ibn al-Qayyim, rahimahullaah, amesema: “Ilhaad [katika majina matukufu na sifa zote njema za Allaah] inatokea ama:

Kwa kukana na kuyakataa majina na sifa Zake; kuyakataa kwa kubadilisha maana yake halisi; kuyafananisha katika maana yake (ta’weelaat); ama kwa kutoa majina ya Allaah kwa vile alivyoviumba kama vile baadhi ya waja waliokwenda kinyume ambao wanaamini kwamba Allah anaweza kuingia katika nafsi ya binadamu (ahlul-ittihaad), kwa sababu wanatoa majina ya Allah kwa vile alivyoviumba japo ni vyakutukuzwa au ni vitu dhalili (Badaa’i’ul-Fawaa’id (1/169); Fathud-Majeed (2/742-743)).

Hivyo basi yeyote yule mwenye kufanya *ilhaad* katika majina na sifa za Allaah, ama kwa kubadilisha maana zake halisi (ta’teel), au kufananisha na viumbe (ta‘weel) au kwa kuyakana (rafd) – kama vile walivyofanya Jahmiyyah, Mu’tazilah na Ash’arees – basi kwa hakika atakuwa amekwenda kinyume na kalima ya laa ilaaha illallaah na kila kinachoelekeza. Hii ni kwa sababu ili kujikurubisha zaidi kwa Yule anayestahiki kuabudiwa (yatawassalu) hakuna budi isipokuwa kwa kutumia majina Yake.

Allaah aliyekuwa juu kabisa amesema kuhusu haya:

“**basi muombeni kwa hayo.” (Soorah aI-A’raaf 7:180)**

Kwa mantiki hiyo basi, ikiwa anayeabudiwa hana majina wala sifa, vipi atakuwa na sifa ya kuabudiwa? Na vipi waja watamwita? Na watamwita kwa majina gani?

Imaam as-Sa’dee, rahimahullah, amesema katika al-Qawlus-Sadeed (uk. 161-163), alipoelezea aya iliyotangulia hapo juu: “Msingi wa tawheed ni kukubali kwa yakini kile chochote Allaah alichojielezea kuhusu Yeye, ama chochote kile mtume wake alivyomwelezea Yeye, juu ya majina Yake mazuri, huku mja akifahamu yanamaanisha nini na yanatoa sifa gani bora juu Yake Yeye. Kumwabudu Allah na kumtaja kwa kutumia majina yake. Na kutokana na ufahamu huu basi, chochote kile mja anachokihitaji kutoka kwa Mola wake – ama kiwe ni kwa ajili ya maisha yake ama kwa ajili ya dini yake- basi ayaombe hayo kwa kutumia majina kati ya majina Yake bora.

Kwa mfano yeyote yule mwenye shida ya riziki basi na amuombe Mola wake kwa kutumia jina Lake la ar-Razzaaq (Mwenyekuruzuku). Na yule mwenye haja ya kujaliwa rehma na kusamehewa madhambi basi amuombe Mola wake kwa kutmia majina kama

vile: ar-Rahmaan (Mwingi wa rehma), ar-Raheem (Mwenyekutoa rehma), al-Birr (Mwenye Wema). al-Kareem (Mkarimu), al-Afu (Mwenye kutoa msamaha). al-Ghaafoor (Mwenyekusamehe), at-Tawwaab (Mwenye kukubali toba) na mengineo yenye kubeba maana sawa.

Na ni bora zaidi kwani, kumtaja Allaah kwa majina Yake na sifa Zake ni ibada ikiwa mja anafahamu maana yake katika moyo wake kiasi ya kwamba anapoyataja, moyo wake unaathirika na maana yake na unajaa na kile kinachoaminishwa. Kwa mfano ikiwa majina yanaamanisha utukufu, ufahari na kibri, kikuli, basi nafsi lazima iwe na uwoga juu ya Allaah na khofu juu Yake; Na majina yanayomaanisha uzuri, njema, upole, imani na huruma ni lazima yajaze katika nafsi mapenzi juu ya Allaah, kumlilia Yeye tu, kumtukuza na kumshukuru . Na majina yanayoonyesha nguvu, hekma, ufahamu wake, uwezo wake unajaza moyo wake katika ulazima wa kutekeleza matakwa Yake, khofu juu ya adhabu Zake, na umuhimu wa kumnyenyekea Yeye tu. Na majina yanayoonyesha sifa za Allaah katika ufahamu wake, jinsi gani anavyopelekewa habari kwa yote yanayofanyika, jinsi gani hahitaji msaada kutoka kokote katika kutekeleza jambo, anavyoona na kushuhudia, vinafanya nafsi kufahamu kwamba Allaah anashuhudia miendo yote na kutulia kokote na hivyo kunamfanya mja ajilinde na mawazo machafu na nia mbaya. Vile vile majina Yake yenyekuonyesha jinsi gani Allaah amejitosheleza, uwezo wake na Yeye tu ndie mtoaji, kunajaza nafsi ufahamu wa kumtegemea Allaah peke yake na uhitaji wake kwake Yeye, na uhitajio wake wa kurejea Kwake Yeye tu wakati wote katika mazingira yeyote.

Imaam Ibn al-Qayyim (rahimahullah) amesema: “Watu walitofautiana katika matendo na fatawa (ahkaam) nyingi, lakini hata mara moja hawakutofautiana katika hata aya moja inayohusu sifa za Allah; Ila masahaba na waliowafuata walikubaliana katika majina na sifa Zake na wakaziacha kama zinavyojielezea, huku wakiamini maana zake na kuwepo kwake[10].

[10] Aqida na kukubaliana kwa Ahlus-Sunnah wal-Jamaa’ah katika masuala ya kuamini sifa za Allaah zimeelezwa kwa uzuri na ufupi na Imaam at-Tirmidhee, rahimahullah, katika kitabu chake cha Sunan (3/266-268):
“Imeelezewa zaidi ya mtu mmoja kutoka kwa waja wenye ilmu kuhusu hadithi hii na zingine zenye kubeba maana sawa kuhusu sifa za Allaah, kamaa vile hadithi inayoelezea kwamba Allaah subhanAllah wa ta’ala; anashuka katika wingu la kwanza kila usiku: kwamba, amini kwa yakini kuhusu hadithi hizi, na amini kile kinachoelezea, wala usifikirie inakuwa vipi (laa yatawahhamu), wala usiulize ni vipi inafanyika au inaonekana. Hadithi kama hizi (zenye kueleza sifa za Allaah) zimesimuliwa kutoka kwa Maalik ibn Anas, Sufyaan ibn ‘Uyaynah na ‘Abdullaah ibn al-Mubaarak. Na wakasema: “Zichukue kama zilivyo, bila ya kuuliza ni vipi “amirroohaa bilaa kayf.” Huu ni usemi wa waja wenye ilmu kutoka kwa Ahlus-Sunnah wal-Jamaa’ah. Lakini Jahmiyyah, wanazikana hadithi hizi na wanasema huku ni kufananisha (tashbeeh) na viume. Wakati, Allaah, aliyekuwa juu kabisa, ametaja katika sehemu tofauti katika kitabu Chake sifa zake kama vile; Mkono, Kusikia na Kuona, lakini Jahmiyyah wanatoa maana nyingine katika aya hizi ambayo inaonyesha sifa fulani, (ta‘weel) na wanazielezea katika njia ambayo sivyo walivyoelezea waja wenye ilmu . Wanasema (Jahmiyyah) Allaah

Hii inaonyesha ubora wa aya hizo mbili ambazo zimeelezewa na umuhimu wake katika kuzifafanua, kwani ni katika kufahamu kwa usahihi na ukamilifu shahadatain na kushikamana nayo ni sehemu muhimu katika tawheed. Na hii ndio sababu Allaah, aliyekamilika, ambaye Yuko juu kabisa, na mtume wake; kwa uwazi na ukamilifu wameelezea kalima kiasi ya kutoacha nafasi ya kutia wasiwasi au shaka katika hilo. Katika aya zinazohusu sifa za Allaah, watu wote pamoja na wale waliojaliwa ufahamu wa kuchambua aya wanazifahamu kwa misingi yake japo wanaweza wasizifahamu mzizi wake au vipi zipo." (33 Mukhtasar Sawaa'iqul-Mursalah (1/15)).

Ibnul-Qayyim pia amesema: "Inajulikana kwa uhalisi wa mwanadamu (fitrah), na kwa kutumia akili timamu na Vitabu vitukufu yeyote yule atakae kuwa na upungufu wa sifa kamili haiwezekani awe Allaah wa kweli wala awe yule mwenye kuendesha masuala yote wala kuwa ndiye Mfalme Mwenye kudumisha na kuhimili; Bali atakuwa anaupungufu, kasoro na wala hajakamilika, wala atakuwa hastahiki kutukuzwa kikamilifu si tu katika hii dunia hata siku ya kiyama. Hii ni kwa sababu mwenye kustahiki kutukuzwa hapa duniani na kesho akhera ni kwa yule tu mwenye kubeba sifa zilizokamilika na bora kabisa ambazo haziwezi kufananishwa na chochote.

Kutokana na haya waja wema waliotangulia ambao wameandika kuhusu sifa za Allaah kuhusu kuwepo juu kabisa, juu ya viumbe vyote alivyoviumba, na kuhusu Maneno Yake na Kuzungumza kwake- wameviita hivi vitabu: Tawheed. Hii ni kwa sababu kutokubali na kuzikana sifa Zake, na kutoziamini ni kumkana Muumba na Kumkataa. Kwa hakika tawheed inahitaji kukubali kwa yakini zifa zilizokamilika za Allaah huku ukikana kufananisha, kuzikosoa na kuzionyesha kutokamilika kwake (Madaarijus-Saalikeen (1/26).

---

hakumuumba Aadam kwa mikono yake, bali wanasema Mkono wa Allaah unamaanisha Uwezo wake! Ishaaq ibn Ibraaheem [ar-Raahawayyah] amesema: Kufananisha sifa za Allaah (tashbeeh) ni pale mja atakaposema : Mkono wa Allaah ni kama mkono wangu, kusikia Kwake na kama vile navyosikia mimi . Lakini mja akisema kama vile Allaah alivyosema: Mkono, Kusikia, Kuona, na kisha haulizi ni vipi hizi sifa zake zipo/zinafanana vipi, wala hasemi Kusikia kwa Allaah ni kama navyosikia mimi basi huku hakumfananishi Allaah na chochote; Bali ni kusema kama vile Allaah aliyetukuka na aliyekuwa juu kabisa alivyosema katika Kitabu chake:

"Hapana kitu kama mfano wake. Naye ni Mwingi wa kusikia Mwingi wa kuona. **"** [Soorah ash-Shooraa 42:11]."

MJA WAKATI ANAPO NUFAIKA KUTOKANA NA KUSHUHUDIA KALIMA YA IMANI

Hapo nyuma tumesema kuwa lazima tunapoitamka laa ilaaha illallaah ni sharti tuwe tunafahamu maana yake na vile vile tuna fuata matakwa yake. Lakini kwa sababu kunauwezekana wa kutofahamu kisawasawa na watu wakaamini kwamba kwa kuitamka tu inatosha kama vile wengine wanavyo dai, hili suala linahitaji kufafanuliwa zaidi ili kufuta upotovu huu kwa wale wenye haja ya kufahamu haki.

Hivyo basi, tukitazama hadithi ya 'Utbaan radiallaahu 'anhu, ambaye amesema: "Kwa hakika, Allaah ameharamisha moto kwa yeyote yule mwenye kusema laa ilaaha illallaah kwa ajili ya kutafuta Uso wa Allaah." (Bukhaaree#425, Muslim #33). Shaykh Sulaymaan ibn 'Abdullaah, rahimahullaah, amesema: "Na fahamu ya kwamba maana ya uwazi wa baadhi ya hadithi kama hizi: ni yeyote yule atakayetamka shahadatain, basi Allaah ataharamisha moto juu yake, kama vile hadithi hii inavyoonyesha na hadithi ya Mu'aadh aliposema:

"Nilikuwa juu ya kipando pamoja na mtume *sallallahu alaihi wasallam* kama msindikizaji, basi akaniambia na akarudia mara tatu: "**Ewe Mu'aadh ibn Jabal!**" Nami nikajibu mara tatu: Nipo hapa, Ewe mtume wa Allaah. Kisha akasema: **"Hakuna mmoja atakayeshuhudia laa ilaaha illallaah muhammadur- rasoolullaah kwa ukweli katika nafsi yake, isipokuwa Allaah atamharamishia moto.** " Nikasema: Ewe mtume wa Allaah, Je niwafahamishe watu ili wapate kupokea habari hizi njema? Akasema: **"Hapana, kwa sababu watategema hili tu.**" Lakini, Mu'aadh akasimulia hadithi hii karibu na kufikwa na mauti, akihofia atakuwa anafanya dhambi (kwa kuficha ilm hii) (al-Bukhaaree , #128).

Nae Muslim amesimulia kutoka kwa 'Ubaadah *radhiyallahu anhu*, kutoka kwa mtume *sallallahu alaihi wasallam*: "Yeyote yule atakaeshuhudia **laa ilaaha illallaah na Muhammad ni mtume wa Allaah, basi Allaah atamkinga na moto juu yake. (Muslim, #47)**

Vile vile kuna baadhi ya hadithi ambazo zinasema yeyote yule mwenyekushuhudia shahadatain ataingia katika bustani ya peponi, lakini hazikusema huyu mtu atakingwa na moto. Kwa mfano hadithi ya Abu Hurayrah – walipokuwa na mtume *sallallahu alaihi wasallam* katika vita vya Tabook – ambayo inasema: **"Hakuna yeyote yule atakayekutana na Allaah huku ameshuhudia laa ilaaha illallaah na mimi ni mtume wa Allaah, bila kuwa shaka juu ya hilo, akazuiwa kuingia katika mabustani ya peponi. (Muslim, #45).**

Bora ya maana zilizosemwa kuhusu maana ya hadithi hii ni kama alivyosema Shaykhul-Islaam [Ibn Taymiyyah] na wengineo: "Hadithi hizi zinamaanisha kwa yeyote yule mwenye kuitamka shahadatain na kisha akafa juu yake, kwa sababu imekuja na masharti yake: kwamba ni lazima itamkwe kwa uyakini katika nafsi, bila ya kuwa na shaka yeyote, na kwa ukweli. Kwa hakika ukweli wa tawheed ni pale nafsi inapokubali na inapovutiwa juu ya Allaah. Hivyo yeyote yule atakeyeshuhudia laa ilaaha illallaah kwa ikhlasi kutoka

katika nafsi yake, ataingia mabustani ya peponi. Hii ni kwa sababu ikhlasi ni kukubali kwa nafsi na kuvutiwa juu ya Allaah, aliyetukuka, kwa kufanya toba kutokana na madhambi mja aliyoyatenda. Hivyo yeyote yule atakayekufa katika hali hii atajaliwa pepo.

Kunao hadithi ambazo zimefikia daraja la juu kabisa kuhusu uhakika wake (mutawaatir), zimenukuliwa kwamba, yeyote yule atakayesema laa ilaaha illallaah, na akawa anayo imani katika moyo wake, hata kama imani hiyo ni ndogo kiasi cha mbegu ya ngano, au ya mbegu ya haradali, au ya atomi – atatolewa motoni. Imesimuliwa pia mara kwa mara katika hadithi zenye daraja hii (mutawaatir) zenye kubeba maana sawa, wengi wenye kusema laa ilaaha illallaah wataingia motoni, lakina iko siku watatolewa motoni. Na pia imesimuliwa katika hadithi za mutawaatir, kwamba, Allaah ameharamisha moto katika sehemu wanazosujudia kwa watoto wa Aadam; ambao walikuwa wanasali na kumsujudia Allaah. Pia imesimuliwa katika hadithi za daraja la mutawaatir kwamba, moto umeharamishwa kwa yeyote yule mwenye kusema laa ilaaha illallaah au mwenye kushuhudia laa ilaaha illallaahu muhammadur-rasoolullaah. Lakini hadithi hizi zimekuja na masharti yake yenye kubeba uzito wake, kwamba wale wenye kuitamka lakini hawafahamu ikhlasi na uyakini unaotakikana kuhusu kalima, basi inakhofiwa kwamba kunauwezekano wakapewa mtihani wakati wa mauti yao na wakashindwa kutamka kalima hii. Kwa hakika, watu wengi wanaotiwa katika mitihani hii wakati wa mauti yao au makaburini ni watu wa aina hii (ambao wanaitamka kalima bila ya ikhlasi na uyakini katika nafsi zao); kama vile hadithi hii ilivyooenyesha:

“Nimesikia watu wakisema usemi fulani, name nikasema kama wao” (Hasan: Sehemu ya hadithi refu iliyosimuliwa na at-Tirmidhee, #737, kutoka kwa Abu Hurayrah *radhiyallahu anhu*. Shaykh al-Albaanee ameiithibitisha usahihi wake katika as-Saheehah, #1391).

Hii inatokea kwa wale watu wengi ambao wanafuata ki kichwa kichwa (kitchwa mchunga), bila kufahamu. Ni wale watu ambao wanakwenda sambamba na maneno ya Allaah aliyekuwa juu kabisa:
“Hakika sisi tuliwakuta baba zetu wanashika dini makhsusi, na sisi tunafuata nyayo zao” [Soorah az-Zukhruf 43:23]

Hivyo basi, hakuna mgongano katika hadithi hizi; kwa sababu kama laa ilaaha illallaah itasemwa kwa uyakini, hakutakuwa na hali ya kuendelea kufanya madhambi. Kwa hakika ikhlas kamili na uyakini usiokuwa na shaka unasababisha mja kumpenda Allaah kuliko chochote kile, na hivyo atakuwa hana hamu ya kufanya mambo ambayo yanamchukiza Allaah, wala atakuwa hana chuki katika kutekeleza yale ambayo Allaah ameyaamrisha. Na huyu ndiye yule ambaye moto utaharamishwa kwake, hata kama alikuwa amefanya madhambi hapo nyuma. Kwa sababu imani hii, kutubu huku kwa ukweli, na ikhlasi hii na mapenzi ya kweli na uyakini, hayabakishi dhambi yeyote kwa mja huyu bali yatafuta madhambi yote kama vile usiku unavyofunika machana” Mwisho wa kunukuu maneno ya sheikh, rahimahullaah. (Tayseerul-Azeezul-Hameed, uk 61-62).

Shaykh Muhammad ibn ‘Abdul-Wahhaab amesema: “Kuna mtafaruku mwingine ambao umejitokeza. Waja wengine wanasema, mtume *sallallahu alaihi wasallam* alimkemea Usaamah kwa sababu ya kumuua mtu mmoja baada ya kutamka laa ilaaha illallaah, na mtume akasema: “Umemua huyu mtu baada ya kutamka laa ilaaha illallaah!”(Bukhari, #4269, Muslim, #159). Na kuna hadithi nyingine ambazo zinazungumzia kumwacha huru anayetamka kalima.

Ufahamu wa huyu jahiliyyah (asiyekuwa na ufahamu sahihi) ni kwamba yeyote yule anayetamka kalima basi hairuhusiwi kuwakufurisha kwa kuwaita makafiri, wala hairuhusiwi kupigana nao- hata kama wanakwenda kinyume na sheriah za Allaah! Hivyo kwa huyu mjinga anaambiwa: Inafahamika kwamba mtume sallallaahu ‘alayhi wa sallam alipigana na mayahudi na kuwashika mateka, japo walikuwa wameitamka kalima ya laa ilaaha illallaah. Na masahaba wa mtume sallallaahu ‘ala yhi wa sallam walipigana na Banoo Haneefah, japo walishuhudia laa ilaaha illallaahu muhammadurrasoolullaah, na walikuwa wanasali na wakisema wao ni waislamu[1]

Vile vile ni katika kisa cha ‘Alee ibn Abee Taalib ambaye aliwachoma baadhi ya watu wakiwa hai. (Bukhari, #6922).

Lakini wakati huo huo, huyu jahil (mjinga, asiyekuwa na ufahamu sahihi) anaamini kwamba yeyote yule ambaye atakana na haamini kuwepo kwa siku ya mwisho basi yeye anastahiki kuitwa kafiri na kuuwawa, hata kama amesema laa ilaaha illallaah. Pia wanaamini kwamba yeyote yule atakayekana nguzo yeyote ya kiislamu anastahiki pia kuitwa kafiri na kuuwawa, hata kama ameitamka kalima. Sasa inakuwaje basi, yule mja anayekana misingi mingine ya uislamu hanufaiki na kalima na inamnufaisha yule ambaye anaikana tawheed; ambayo ndiyo kiini cha dini mitume walichotumwa nacho? Kwa hakika, maadui wa Allaah hawaifahamu maana sahihi za hadithi hizi. (Kashfush-Shubuhaat, uk 45-49).

Sheikh, rahimahullaah, pia amesema: “Na vipi inatakikana kuifahamu hadithi ya Usaamah ambaye alimuua mmojawapo wa makafiri baada ya kushuhudia kuwa yeye ni muislamu, ni kwa sababu usaamah alifikiria kwamba alishuhudia tu kwa kuhofia maisha na mali yake. Hivyo basi, itakapotokea mtu yeyote anashuhudia kuwa yeye ni muislamu kwa dhahiri, basi ni wajibu kuacha kumpiga vita, mpaka ifahamike kwa uwazi amefanya jambo ambalo linamtuo katika uislamu (Jambo ambalo inakuwa wajibu kumpiga vita).

Allaah ameteremsha wahyi kuhusu suala hili kwa kusema:
“Enyi mlio amini! Mnapo toka kwa ajili ya kupigania njia ya Allaah basi hakikisheni, wala msimwambie anaye kutoleeni salamu: Wewe si Muumini.” [Soorah an-Nisaa 4:94]

Hivyo, aya hii inashuhudia wajibu wa kutompiga vita muislamu yeyote mpaka uthibitisho wa uhakika upatikane. Na kama uthibitisho ukipatikana ya kwamba mja anakwenda kinyume na uislamu, baada ya kufanya uchunguzi basi huyo mja anastahiki kupigwa vita kwa sababu hilo ndilo amrisho la Allaah baada ya kuthibitisha. Na kama ingekuwa

kwamba mja hapigwi vita baada ya kutamka kalima, basi amri ya kuthibitisha ukweli ingekuwa haina maana!

Vile vile, pia katika hadithi nyingine ambazo tumeshazisema zinazobeba maana sawa ya kwamba, yeyote yule anayeonekana kidhahiri ni muislamu na mwenye kufuata tawheed, basi ni wajibu kutompiga vita, labda ifahamike wazi kwamba anakwenda kinyume na matakwa ya uislamu. Na dalili juu ya hili ni hadithi ya mtume *sallallahu alaihi wasallam* amesema:

> "Umemuua baada ya yeye kutamka laa ilaaha illallaah!"

Na tena amesema:

> "Nimeamrishwa kuwapiga vita watu mpaka wakiri kuwa hakuna apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allahh." (Bukhari, # 392, Muslim, #35).

---

[1]Kisa hiki kilitokea wakati Banoo Haneefah waliporitadi chini ya uongozi wa aliyekuwa anadai yeye ni mtume, Musaylamah. Masahaba waliwapiga vita katika vita vya Yamaamah, wakati wa uongozi wa Aboo Bakr radiallaahu 'anhu, mwaka 11H. Rejea al-Kaamil (2/218-224) ya Ibn al-Atheer.

Na pia ni yeye pia (mtume sallallahu alaihi wasallam) aliyesema kuhusu Khawaarij:

> "Na kama nikikutana nao basi nitawaua, kama vile jamii ya Aad ilivyo uliwa." (Bukhaaree, #6930, an Nasaa'ee, # 3823)

Na hivi ndivyo ilivyokuwa, japo walikuwa wakitamka mara kwa mara laa ilaaha illallaah, kiasi kuwafanya masahaba waone ibada zao si chochote kufananisha na zao (khawaarij). Khawaarij pia walikuwa ni wamojawapo waliokuwa wamesoma ilmu kutoka kwa masahaba, na bado huko kutamka kwao laa ilaaha illallaah hakukuwanufaisha chochote wala hawakuacha ibada zao wala uislamu wao- kwa sababu walionyesha matendo ambayo ni kinyume na sheria za kiislamu. Vile vile katika suala la kuwapiga vita mayahudi na Banoo Haneefah, kama tulivyo taja hapo nyuma (kashfush-Shubuhaat, uk 49-51).

Al-Haafidh Ibn Rajab amesema katika jarida lake lenye kichwa cha habari Kalimatul-Ikhlaas (uk.20-21), alipokuwa anatoa maelezo ya ziada kuhusu hadithi ya mtume *sallallahu alaihi wasallam*:

> Nimearishwa nipigane na watu, mpaka wa shuhudie laa ilaaha illallaah (hapana apasae kuabudiwa kwa haki ila Allaah) na mimi ni mtume wa Allaah, na wasimamishe sala na watoe zaka." (Imesimuliwa na Bukhari#25, Muslim, #36, kutoka kwa Ibn Umar)

kwamba: " 'Umar na baadhi ya masahaba walifahamu kutoka katika hadithi hii kwamba yeyote yule atakayetamka shahaadatain, atalindwa na adhabu za hapa duniani. Basi wakawa hawapigani na wale waliokataa kutoa zakaah. Lakini, [Abu Bakr] as-Siddeeq alifahamu kutoka katika hadithi hii kwamba kupingana nao kusizuilike mpaka watimize haki za kalima, kutokana na usemi wa mtume sallallaahu 'alayhi wa sallam:

> "Na kama wakifanya hivi basi, damu yao na mali zao zitalindwa kutoka kwangu, isipokuwa kwa kile kiwango ambacho ni haki katika uislamu, na hesabu yao iko kwa Allaah." (Mwisho wa hadithi iliyotangulia)
>
> Abu Bakr amesema: "Zakaah ni haki ambayo iko juu ya mali." (Bukhari, #1400)

Ufahamu huu wa Abu Bakr as-Siddeeq umebobea katika masimulizi ya wazi kutoka kwa mtume *sallallahu alaihi wasallam* kutoka kwa zaidi ya sahaba mmoja – ambayo unawajumuisha – Ibn 'Umar, Anas na wengineo – kwamba alisema:

> "Nimearishwa nipigane na watu mpaka wa shuhudie laa ilaaha illallaah na mimi ni mtume wa Allaah, na wasimamishe sala na watoe Zakaah."

Hii pia imeshuhudiwa na Allaah aliyekuwa juu kabisa pale aliposema:

"So if they repent (from their unbelief), establish the Prayer and give the Zakaah, then leave their way free." [Soorah at-Tawbah 9:5]

Katika aya nyingine yenye maana sawa:

"Basi wakitubia, na kusamisha sala, na kutoa zakaah, basi watakuwa ni ndugu zenu katika dini." [Soorah at-Tawbah 9:11]

…ina hakikisha undugu katika uislamu hausimamishwi isipokuwa kwa kutimiza mambo ambayo ni wajibu huku tawheed ikiwa imekubalika. Kwa hakika toba ya kujinosoa katika shirki haitafanikiwa isipokuwa kwa kukubali kwa yakini tawheed. Hivyo, pale Abu Bakr alipokubaliana na masahaba, walikubali usemi wake na wakaona hoja yake imesimama katika haki. Hivyo basi, sasa unafahamu ya kwamba, adhabu haiachwi kwa mja wa kiislamu kwa sababu tu ametamka shahadatain ila mja wa kiislamu anaweza akapata adhabu kwa sababu ya mapungufu katika kutekeleza masharti na haki katika dini (Islaam), na vile vile kutakuwa na adhabu pia kesho siku ya kiyama."

Ibn Rajab amesema pia: "Baadhi ya maulamaa wamesema maana ya hadithi hizi zinazosema laa ilaaha illallaah ni sababu ya kuingia katika mabustani ya peponi, na kukingwa na moto na kwamba inafanya wajibu kwa yule aliyotamka kuingia peponi. Lakini matokeo hayo (ya kuingia peponi) hayapatikani mpaka shurti (shuroot) zake zitimizwe na upungufu (intifaa'ul-muwaani') wowote uondolewe. Na ikiwa hayatatekelezwa haya, basi kuna uwezekano, wa kuzuiwa kuzawadiwa kutokana na ukosefu wa sharti mojawapo au kwa kuwepo kwa mojawapo ya upungufu. Hivi ndivyo alivyosema al-Hasan (al-Basree) na Wahb ibn Munabbih na ndio hoja inayobeba nguvu zaidi.

Al-Hasan alimwambia al-Farazdaq, wakati akimzika mke wake: "Umetayarisha nini katika siku kama hii?" Akajibu: Kushuhudia kwa Allaah, laa ilaaha illallaah katika miaka sabini ya uhai wangu. Al-Hasan akasema: "Mtayarisho gani mzuri huo, Lakini, laa

ilaaha illallaah ina shurti zake, hivyo kuwa makini na kumsingizia mwanamke mwenye kustiri tupu yake."

Pia kuna mara al-Hasan aliambiwa: Kuna baadhi ya watu wanafikiri kwamba yeyote yule atakayesema laa ilaaha illallaah ataingia katika mabustani ya peponi. Basi akajibu: Yeyote yule atakayesema laa ilaaha illallaah, akatimiza haki zake na matakwa yake, ataingia katika mabustani ya peponi.

Nae Wahb ibn Munabbih mara aliulizwa: Je sio laa ilaaha illallaah ni ufunguo wa peponi? akajibu: "Kwa hakika, lakini hakuna ufunguo usiokuwa na meno. Basi yeyote yule atakayekuwa amebeba ufunguo ukiwa unao meno yake basi atafunguliwa mlango. Na kama ufunguo huo utakuwa hauna meno, basi hatafunguliwa!" (Bukhari, 3/141) (Kalimatul-Ikhlaas (uk.15-17).

Naamini kwamba ninaponukuu kutoka kwa waja waliojaliwa ilm inatosha kuondoa shaka kwa wale wenye kuamini kwamba yeyote yule mwenye kutamka laa ilaaha illallaah haiwezekani hata siku moja waitwe makafiri, hata kama anafanya mambo ambayo ni shirk kubwa, ambayo yanafanyika hata siku hizi katika makaburi ya waja wema; matendo ambayo yanapinga na kwenda kinyume na kalima laa ilaaha illallaah. Na ufahamu huu umechukuliwa na wanaokwenda kinyume na dini, ambao wanachukua maandiko yenye kubeba maana ya juu katika jambo na kisha wakazisimamisha kama dalili zao na wanacha maandiko mengine ambayo yanaelezea na kufafanua zaidi hukumu ya jambo hilo. Hawa ni sawa na wale wenye kuamini baadhi ya sehemu ya Kitabu na wanakana baadhi ya sehemu katika Kitabu. Allaah amesema kuhusu watu hawa:

"Yeye ndiye aliye kuteremshia Kitabu hichi. Ndani yake zimo Aya muhkam, zenye maana wazi (almuhkamaait). Hizo ndizo msingi wa Kitabu hichi. Na ziko nyengine ambazo si za wazi (almutashaabihaat). Ama wale ambao nyoyoni mwao umo upotovu wanafuata zile za ambazo haziko wazi kwa kutafuta fitna, na kutafuta maana yake; na wala hapana ajuaye maana yake ila Allaah. Na wale wenye msingi madhubuti katika ilimu husema: Sisi tumeziamini, zote zimetoka kwa Mola wetu Mlezi. Lakini hawakumbuki hayo isipo kuwa wenye akili. (Na hao husema): Mola wetu Mlezi! Usizipotoe nyoyo zetu baada ya kwisha tuongoa, na utupe rehema itokayo kwako. Hakika Wewe ndiye Mpaji. Mola wetu Mlezi! Wewe ndiye Mkusanyaji wa watu kwa Siku isiyo na shaka ndani yake. Hakika Allaah havunji miadi yake." [Soorah Aal-'Imraan 3:7-9][2].

Ewe Allaah! Tuonyesha haki na utajalie ni wenye kufuata; na tuonyeshe batili na utujalie tuwe ni wenye kuitambua na kuiepuka.

[2]Imaam ash-Shaatibee, rahimahullaah, amesema katika kitabu chake bora kabisa at-I'tisaam (1/231): "Yeyote yule atakayefuata aya ambazo haziko wazi (mutashaabihaat aya); akageuza maana halisi (ya aya) ; akatoa maana ambayo hajatolewa na waja wema waliotangulia (Salafus-Saalih); akashikamana ha hadithi ambazo ni dhaifu na zimetungwa, au akatumia maana ambayo ni ya juu, ili kukubaliana na lengo na nia yake [kithabiti] bila ya kutafuta dalili za msingi katika kufahamu jamb- basi hii ni njia ambayo inapelekea kwenye mambo ya uzushi na wazushi (bida'a na mubtadia).

ATHARI ZA KALIMA YA IMANI KWA MJA NA JAMII KWA UJUMLA

Kama hii kalima itatamkwa kwa ukweli na ikhlasi na matakwa yake yakatekelezwa kidhahiri na kisiri basi kwa hakika athari yake kwa mja mwenyewe na kwa jamii kwa ujumla itakuwa ni yenye kusifika. Mojawapo ya sifa bora za athari ya kalima ni:

1- Kuwa na kauli moja ambayo itawasaidia waislamu kuwa na nguvu na ushindi zidi ya maadui zao. Hili litafanikiwa kwa sababu watakuwa wanafuata dini moja na imani (‘aqeedah) moja kama Allaah aliyekuwa juu kabisa alivyosema:

“Na shikamaneni na Kamba ya Allah nyote pamoja, wala msifarikiane..” [Soorah Aal-’Imraan 3:103]

Na Allaah aliyetukuka amesema pia:

“Kwani Yeye ndiye aliye kuunga mkono kwa nusura yake na kwa Waumini.
Na akaziunga nyoyo zao kwa mapenzi. Na lau wewe ungeli toa vyote viliomo duniani usingeli weza kuziunga nyoyo zao kwa mapenzi, lakini Allah ndiye aliye waunganisha. Hakika Yeye ndiye Mtukufu Mwenye nguvu na Mwenye hikima.” [Soorah al-Anfaal 8:62- 63]

Na kutafautiana katika aqeedah kunasababisha mgawanyiko, mfarakano, chuki- Kama alivyosema Allaah mtukufu:

“Hakika walio igawa Dini yao na wakawa makundi makundi, huna ukhusiano nao wowote.” [Soorah al-An’aam 6:159]

Na tena Allaah alieyekuwa juu kabisa amesema:

“Lakini watu walikatiana jambo lao la umoja katika makundi mbali mbali. Kila kundi likifurahia kwa waliyo nayo.” [Soorah al-Mu’minoon 23:53]

Hivyo basi watu hawawezi wakaungana mpaka wawe na itikadi sawa katika imani (eemaan) na tawheed; ambayo ndiyo maana ya utekelezaji wa laa ilaaha illallaah – na hili linathibitishwa na jinsi waarabu walivyokuwa kabla na baada ya uislamu.

2- Katika jamii inayoikubali tawheed na inafuata matakwa ya laa ilaaha illallaah inakuwa na usalama na utulivu.

Hii ni kwa sababu kila mja atakuwa anafanya na kutekeleza yale ambayo ni halali na ataacha yale ambayo Allaah ameyakataza, na anafanya hivyo ili kutimiza matakwa ya kalima. Hivyo basi atajizuia hasira, kutotenda haki na dhuluma na badala yake atakuwa na ushirikiano, mapenzi na kushikamana kwa ajili ya Allaah; akatekeleza usemi wa Allaah:

“Hakika Waumini ni ndugu” [Soorah alHujuraat 49:10]

Hili limeonekana wazi kwa waarabu katika maisha yao kabla ya kuikubali na kuwa tayari kutekeleza matakwa ya kalima na baada ya kuikubali na kujisalimisha katika utekelezaji wa matakwa ya kalima. Kabla ya kujisalimisha juu ya kalima, walikuwa ni maadui baina yao, wakichinjana wenyewe kwa wenyewe, wakijisifu jinsi gani wanaua, kupora na kuharibu mali. Lakini walipojisalimisha juu yake, wakawa kama ndugu ambao wanamapenzi baina yao. Allaah aliyetukuka amesema:

“Muhammad ni Mtume wa Allaah. Na walio pamoja naye wana chuki na ukali mbele ya makafiri, na wana upendo na huruma wao kwa wo.” [Soorah al-Fath 48:29]

Na Allaah aliyekuwa juu kabisa amesema:

“Na kumbukeni neema ya Allaah iliyo juu yenu: vile mlivyo kuwa nyinyi kwa nyinyi maadui naye akaziunganisha nyoyo zenu kwa mapenzi; kwa neema yake mkawa ndugu.” [Soorah Aal-’Imraan 3:103]

3- Kuongoza na kurithisha uongozi (khilaafah) katika dunia, na kulinda usafi wa dini na uimara/ukakamavu katika mawazo na hoja potovu ; kama alivyosema Allaah, aliyetukuka:

“Allaah amewaahidi wale walio amini miongoni mwenu na wakatenda mema kwa makutii Allaah na mtume wake, ya kwamba atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyo wafanya makhalifa wa kabla yao, na kwa yakini atawasimamishia Dini yao aliyo wapendelea, na kuwawezesha kufauata dini ambayo amewachagulia na ndio aliyowaamrisha. Na atawabadilishia amani baada ya khofu yao ikiwa wata wananiabudu Mimi, watanitii Mimi wala wasinishirikishe na chochote katika ibada.” [Soorah an- Noor 24:55].

Hivyo tunaona Allaah amefahamisha upatikanaji wa haya malengo makuu hayapatikani ila kwa kusafisha dini kwa ajili ya Allaah peke yake bila ya kumshirikisha na chochote. Na hii ndiyo maana na matakwa ya laa illaaha illallaah.

4- Kufanikiwa kupata usalama na utulivu wa nafsi, vile vile kupata utulivu wa akili na utulivu wa kisaikologia kwa yeyote yule anayesema laa ilaaha illallaah na akafuata matakwa yake.

Hii ni kwa sababu mja huyu ni mtumwa na mwenye kumwabudu Allaah peke yake. Anafahamu Mola wake anataka nini na yapi yanamfurahisha, hivyo anayatekeleza. Vile vile, anafahamu yapi yanamkasirisha Allaah na anayaaacha.

Na hii ni tafauti na yule ambaye anaabudu na ni mtumwa zaidi ya mungu mmoja, kila mmoja anataka afanye jambo ambalo wengine hawataki. Na vile vile kila mmoja anapanga mipangilio tofauti. Allaah, aliyekuwa juu kabisa amesema:

“Je, mabwana wengi wanao farikiana wao kwa wao ni bora au Allaah Mmoja Mwenye nguvu?” [Soorah Yoosuf 12:39]

Na tena Allaah aliyekuwa juu kabisa amesema:

“Allaah amepiga mfano wa mtu mwenye mabwana washirika wanao gombana, na wa mtu mwengine aliye khusika na bwana mmoja tu. Je! Wako sawa katika hali zao?” [Soorah az-Zumar 39:29]

Imaam Ibnul-Qayyim amedokeza: “Mfano huu ambao Allaah aliyekamilika ameotoa, ni kama mfano wa mja mwenye kuabudu zaidi ya Allaah (Mushrik) na mwenye kumwabudu Allaah peke yake (Muwahhid). Basi mfano wa mshirikina (mushrik) ni kama yule mtumwa anaye milikiwa na mabwana zaidi ya mmoja ambao wakati wote wanapingana, wanabishana na wanaonyeshana chuki kati yao; hivyo mja anakuwa dhalili.

Hivyo basi kwa sababu mshirikina ni yule anayeabudu miiungu tofauti, amafananishwa na yule mwenye kutawaliwa na mabwana zaidi ya mmoja ambao wanashindana katika kumfanya afanye kazi na awe mtiifu juu yao. Na haiwezakani awaridhishe wote!

Kwa upande mwingine, mfano wa muwahhid ambaye anamwabudu Allaah peke yake, ni sawa na mtumwa mwenye bwana mmoja anayetakikana kuwa mtiifu juu yake. Mtumwa huyu anajua bwana wake anataka nini na anajua atumie njia gani ili apate kumridhisha. Hivyo anakuwa hana malumbano wa mambo ambayo yatamchanganya (tofauti na angekuwa na mabwana zaidi ya mmoja, kwani malumbano au kuchanganyikiwa kungekuwepo). Bali atakuwa salama kwa bwana wake, bila ya kuwa na mtafaruku nani amuhudumie na amtii, na wakati huo huo, bwana wake anamuonyesha upole, huruma na ukarimu, akimfanyia mambo mazuri na kumtekelezea yanayomfurahisha. Je hawa watumwa wako sawa?” (I’laamul-Muwaqqi’een (1/187).

5- **Kupata adhima na utukufu hapa duniani na kesho akhera**, kwa waja wa wanayoitamka laa ilaaha illallaah.

Allaah aliyekuwa juu kabisa amesema:

“Kwa kumtakasikia Imani Allaah, peke yake bila ya kumshirikisha. Na yeyote yule anaye mshirikisha Allaah ni kama kwamba ameporomoka kutoka mbinguni, kisha ndege wakamnyakua au upepo ukamtupa pahala mbali” [Soorah al-Hajj 22:31]

Aya hii inathibitisha tawheed ni jambo bora kabisa na lenye kupaa juu kabisa , wakati shirki ni jambo dhalili na lenye kudhalilisha.

Ulamaa mshuhuri, Ibn al-Qayyim, rahimahullaah, amesema: “Allaah amefananisha daraja, ukubwa na ubora wa imani na tawheed kama mbingu ambayo ndio sehemu mambo yakapaa na mengine yakashuka. Kutoka kwake (mbingu) imani na tawheed inashuka katika ardhi na vile vile inapaa kwake.

Kukana imani na tawheed kumefananishwa kama kuporomoka kutoka mbinguni kwenda kwenye sehemu ya chini kabisa ya sehemu dhalili; kama vile moyo unavyokunjamana na kuwa na maumivu yaliyojikusanya ambayo hayaishi. Na ndege ambao wananyafua nyama kutoka katika miguu yake na wakasababisha uharibifu ni sawa na shetani ambaye Allaah amemtuma kumpeleka mja katika maovu, kumnyanyasa na kumtamanisha kwenda kwenye sehemu ambazo zitamsabibasha kupotea. Na Upepo ambao unampeperusha mbali kabisa ni sawa na matamanio ya nafsi yake ambayo yamempeleka sehemu dhalili kabisa, mbali na peponi (I'laamul-Muwaqqi'een (1/180)).

6- Kuchunga damu, mali na utu wa kila mja muislamu, kama alivyosema mtume *sallallahu alaihi wasallam*:

"Nimearishwa nipagane na watu mpaka waseme laa ilaaha illallaah. Na wakisema hivyo, basi damu na mali zao zitalindwa, labda tu; wakishindwa kutimiza haki zake, na malipo yao yapo juu ya Allaah" (al-Bukhaaree (13/419).

Na kama wakisema lakini wakafeli katika kutimiza haki zake- ambayo inamaanisha wakafeli kumkwepesha Allaah peke yake katika ibada na wakawa kwa uwazi wanaabudu vingene pasipokuwa Allaah, na wakafeli kusimamisha nguzo za uislamu- basi mali na damu zao hazistahiki kulindwa, na wanastahiki kupigwa vita, na mali zao kuchukuliwa kisha wakapewa waislamu kama ngawira, kama vile mtume *sallallahu alaihi wasallam* na wale waliomfuatia walivyofanya.

Kwa hayo, tunamalizia kwa kusema, kalima hii ina athari kubwa kwa kila mja na jamii kwa ujumla, ikiwa katika ibada, biashara, hulka na tabia. Na kufaulu kunategea kwa Allaah. Na tunamuomba Allaah ampandeshe darja na rehma na amani zimshukie mtume Muhammad; familia yake, masahabha zake na wale wote wenye kumfuata